
# Nipashe

Jumatano Oktoba 30, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580062
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Waliotumbuliwa na vyeti feki wabuni mbinu kupata mafao

UKURASA 3


UJIKUMBUSHE
Kiongozi wa IS aliyeuawa na Marekani Ukurasa 18
Mafunzo yanavyohamasisha wanawake kuwania uongozi Ukurasa 15
siasa
JUMATANO OKTOBA 30, 2019 Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
JAMES MAPALALA, mwanasiasa ambaye hakukata tamaa Ukurasa 14
Wenye ulemavu na uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa
• Washauri watengewe nafasi maalumu za kugombea ndani ya vyama
• Wadau washauri serikali iwatengee bajeti maalumu
Na Elizabeth Zaya
BAADA ya kumalizika kwa muda wa uandikishwaji katika orodha ya wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Chama cha Wasioona (TLB) kimetoa maoni yao, huku kikipendekeza kuboresha utaratibu wa namna ya kutoa vipaumbele kwa watu wenye ulemavu katika shughuli za namna hiyo.
Rehema Hamis Darueshi ni Mratibu Idara ya Wanawake na Watoto wa Chama hicho.
Anasema bado hakuna utaratibu wa kuwatambua watu wenye ulemavu katika ngazi ya Serikali
INAENDELEA UK.16
Mfumo wa Iran uliowekwa Iraq, Lebanon waanza kusambaratika Ukurasa 20
Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo. PICHA: MTANDAO
Vyama vilivyojipanga Kilimanjaro kushinda katika chaguzi zijazo Ukurasa 19

UKURASA 13

# Waziri Kangi Lugola awa trafiki wa muda

**• Asimamisha** basi na kupoka leseni ya dereva, aagiza apelekwe lupango, abiria warejeshewa nauli... *Ukurasa 2*




Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (kulia), akimhoji dereva wa basi la abiria la Manoni Safari, Marijani Said (kushoto), ambaye alitaka kusababisha ajali kutokana na mwendo kasi huku akilazimisha kulipita gari lingine katika Kijiji cha Nyashishi, wilayani Busega, Mkoa wa Simiyu jana. **PICHA: WMNN**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**MVUA NYINGI KUHAMIA MIKOA KANDA YA ZIWA**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema mikoa ya Kanda ya Ziwa itakuwa na mvua nyingi na...

**UKURASA WA 3**

**MSHTAKIWA KESI VIGOGO WA NIDA AJISALIMISHA KWA DPP**

XAVERY Silverius, anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ameandika barua kwa Mkurugenzi wa...

## Chadema yalia rafu uchaguzi wa mitaa

UKURASA 3

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

# Kiharusi tishio vifo vya watu

**• Ni** cha pili duniani baada ya moyo, Muhimbili yapokea wagonjwa watano kwa siku... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** ZAHERA AISHUKIA YANGA KUTIMULIWA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri Lugola ageuka trafiki

**Na Felix Mwagara,** BUSEGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameyakamata magari mawili yaliyotaka kusababisha ajali kwa kufukuzana na kulazimisha kuyapita magari mengine bila ya kuwa na tahadhari katika Barabara Kuu ya Mwanza-Mara.

Magari hayo ni basi lililokuwa na abiria liitwalo Manoni Safaris lenye namba za usajili T800 DCU na lori namba T865 CVJ yaliyokuwa yanatokea Mwanza kuelekea mkoani Mara.

Akiwa safarini akitokea wilayani Bunda, waziri huyo alilazimika kuchukua hatua hiyo jana, magari hayo yalipofika katika Kijiji cha Nyashishi wilayani Busega mkoani Simiyu yakidaiwa kuwa kwenye mwendokasi.

Ilielezwa kuwa baada ya kushuhudia magari hayo yakiwa katika mwendokasi na yanalazimika kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari, waziri huyo alimtaka dereva wake kugeuza gari na kuyafuatilia magari hayo.

"Huyu dereva wa basi hana tahadhari na ni mtu hatari sana, alitaka kutuua na pia kuua abiria wa basi hili, lazima afunguliwe mashtaka apelekwe mahakamani na iwe fundisho kwa madereva wazembe wa aina hii, na nimeambiwa na abiria hapa kuwa aliwapuuza baada ya kuambiwa apunguze mwendo," alisema Lugola baada ya kulisimamisha basi hilo.

Waziri huyo alimkamata dereva wa basi hilo, Marijani Saidi, na kumtaka atoe leseni yake na baadaye alipelekwa Kituo cha Polisi Busega ili kukamilisha taratibu za kufunguliwa mashtaka.

Waziri huyo pia aliagiza abiria wa basi hilo warudishiwe nauli zao na watafutiwe basi lingine ili waendelee na safari.

Akizungumzia tukio hilo, abiria wa basi hilo, Mwita Machela, alidai walimtaka dereva huyo kuacha kuendesha kwa mwendokasi, lakini aliwapuuza na kuendelea na safari.

"Waziri yuko sahihi kutusimamisha maana ametuokoa pia, huyu dereva alikua mwendokasi, tulimwonya aache, lakini hakutusikiliza, sasa haraka yake imeishia hapa, na sisi tumepotezewa muda wetu kutokana na uzembe wake," alisema.

Waziri Lugola pia alimsimamia kondakta wa basi hilo akiwarudishia nauli abiria hao na kuhakikisha wanapandishwa katika mabasi yaliyokuwa yanapita katika barabara hiyo



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (wa pili kushoto), akifurahia jambo na Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye (wa pili kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku (kulia), Naibu Waziri wa Tamisemi, Mwita Waitara (katikati), Mwenyekiti wa Kituo cha Sera za Kimataifa Afrika, Prof. Rwekaza Mukandala (kushoto), Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania, James Mbatia na viongozi wengine, baada ya kuwasili kwa ajili ya kufungua kongamano la kitaifa la amani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Mvua nyingi kuhamia mikoa Kanda ya Ziwa

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema mikoa ya Kanda ya Ziwa itakuwa na mvua nyingi na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TMA, mikoa itakayokumbwa na mvua hizo ni Geita, Kagera, Mara na Magharibi mwa Simiyu.

Aidha, kiwango cha athari kinachoweza kutokea ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji, ucheleweshaji wa usafiri, kusimama kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Wiki kadhaa zilizopita TMA ilitoa tahadhari ya uwapo wa mvua kwenye mikoa mbalimbali nchini ambayo itaanza Novemba hadi Aprili mwakani.

Aidha, siku chache baadaye Mamlaka hiyo ilitoa utabiri wa mvua kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga.

Tangu kuanza kwa mvua hizo, watu 25 wamepoteza maisha katika mikoa ya Morogoro na Tanga, huku madaraja manne yalisombwa na maji na kukatika kwa mawasiliano kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

# Kiharusi cha pili kwa vifo duniani

**Na Romana Mallya**

UGONJWA wa kiharusi umeelezwa kuwa ni tishio kutokana na kusababisha vifo vya watu duniani na sasa unashika nafasi ya pili baada ya maradhi ya moyo.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa kushika nafasi hiyo kwa asilimia 11.8, imeelezwa kuwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa siku imekuwa ikipokea wagonjwa watatu hadi watano wenye kiharusi.

Sambamba na hilo, imeelezwa kuwa kwa upande wa watoto, takwimu za wagonjwa wa ndani zilizoanzia Julai, mwaka jana hadi Julai, mwaka huu, watoto waliogundulika kuwa na kiharusi chini ya miaka 14 ni 23.Wakizungumza jana kwa nyakati tofauti wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kiharusi Duniani, madaktari bingwa wa hospitali hiyo walisema ugonjwa huo ni wa tatu unaosababisha ulemavu kwa asilimia 4.5 ya walemavu duniani.

Daktari Bingwa wa Mishipa ya Fahamu, Ubongo na Uti wa Mgongo, Patience Njenje, alisema kiharusi ni moja ya magonjwa ambayo si ya kuambukiza lakini akasisitiza: "Kwa siku watu wazima wanaopokewa Muhimbili, wagonjwa watatu mpaka watano wana kiharusi."

Akielezea chanzo cha ugonjwa huo, Dk. Njenje alisema mtu anapata kiharusi pale ubongo unapokosa hewa na chakula ambacho ni damu inayosafirishwa kupitia mishipa.

"Kuna wakati mishipa hii huziba au hupasuka. Mtu akipata hali hiyo anaweza kukosa nguvu upande mmoja. Kama imepasuka upande wa kushoto, utakosa nguvu upande wa kulia na madhara makubwa ni kifo au kupata ulemavu," alisema.

Alisema takwimu za sasa za dunia zinaonyesha kiharusi kinashika nafasi ya pili katika kusababisha kifo lakini zamani kilikuwa nafasi ya mbali kidogo. "Maana yake, kiharusi kinazidi kusogea na hatuombei. Kinaweza kuvuka na kupita magonjwa ya moyo. Wengi wanafikiri mtu akipata kiharusi amerogwa, lakini tunataka kuwaelimisha wananchi kuwa matatizo haya yapo na nijukumu la kila mmoja kuchukua tahadhari kwenye mfumo mzima wa maisha.

"Zamani, matatizo ya kiharusi yalikuwa zaidi nchi za Ulaya, lakini sasa inakuja kwa sababu watu wameiga maisha ya Ulaya. Tusiporudi tulikotoka kwa mfumo mzima wa maisha hali itazidi kuwa mbaya," alisema.

Daktari huyo alisema awali ugonjwa huo ulikuwa ukiwapata watu wenye umri wa miaka 65 kuendelea lakini kwa sasa wenye miaka 45 na kushuka chini wanaupata.

Dk. Zameer Fakih, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto, alisema kiharusi kwa watoto kinaweza kutokea kabla ya kuzaliwa, wakati wa kuzaliwa na baada ya kuzaliwa.

"Takwimu zinaonyesha kati ya watoto 4,000 wanaozaliwa, mmoja anapata kiharusi wakati akizaliwa. Chini ya umri wa miaka 18 kila mwaka watoto 2,000 wanapata kiharusi kutokana na sababu mbalimbali. Takwimu hizi ni za utafiti wa dunia nzima," alisema.

Dk. Fakih alisema endapo mtoto anayezaliwa atakosa hewa (oxygen) ana uwezekano wa kupata kiharusi baadaye. "Anaweza kupata degedege ikahusisha upande mmoja wa mwili au mwili mzima au akapata ulemavu upande mmoja akawa anakakamaa upande mmoja. Anaweza kuonyesha dalili za kushindwa kunyonya au kula sawasawa na wakubwa ambao wanaweza kupata dalili za kukata kauli," alisema. Hata hivyo, alisema iwapo mtoto atawahishwa hospitalini chini ya saa sita, matibabu yatakuwa rahisi zaidi na atakapocheleweshwa, athari zitaongezeka.

Dk Fakih alibainisha kuwa watoto ambao wanaweza kupata kiharusi ni wale wenye matatizo ya seli mundu ikifuatiwa na wale wenye matatizo ya valvu za moyo.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ubongo na Mishipa ya Fahamu, Mohamed Mnacho, alisema utafiti unahitajika zaidi ili kupata takwimu za hali ilivyo kwa wakati huu.

Dk. Mnacho alisema utafiti uliofanyika Tanzania na duniani, unaonyesha kwa kiasi kikubwa matatizo ya shinikizo la juu la damu, kisukari, magonjwa ya moyo (valvu za moyo), seli mundu na moyo kutanuka, yanachangia kwa kiasi kikubwa mtu kupata kiharusi.

"Baadhi ya wanawake wakati wa ujauzito hupata kiharusi, ugonjwa huu unatibika kama mgonjwa atafika hospitali kwa wakati," alisema.



Wachuuzi wa Matikiti wakichagua kwa bei ya jumla katika Soko la Vetenari Tazara, jijini Dar es Salaam jana, ili kwenda kuuza mitaani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waliotumbuliwa na vyeti feki wabuni mbinu kupata mafao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATUMISHI wa serikali walioachishwa kazi kwa udanganyifu wa vyeti vya kielimu na taaluma, wamebuni mbinu za kupata mafao.

Imeelezwa kuwa moja ya mbinu zao ni kutumia majina ya walimu waliostaafu miaka ya nyuma.

Mwalimu mstaafu wa Shule ya Msingi Kahama B iliyoko mjini Kahama, Cornel Benedict (65), amefichua mbinu hizo baada ya kunusurika kupoteza mafao yake kutokana na mmoja wa watumishi wa umma kutumia jina lake kuomba kulipwa mafao.

Benedict aliyestaafu mwaka 2016, alisema katika jitihada za kufuatilia mafao yake Halmashauri ya Mji wa Kahama, alibaini kuwapo kwa mtu anayetumia majina yake ya Cornel Benedict na tayari alikuwa kwenye mchakato wa kupatiwa mafao.

Alisema alibaini uwapo wa mtu huyo baada ya kupigiwa simu na watumishi wa halmashauri hiyo na kuelezwa kuwa kuna mtu kajitokeza anatumia majina yake na anahitaji kupatiwa faili lake.

"Nilipigiwa simu na maofisa wa Halmashauri wa Idara ya Elimu wakiniambia kuna mtu anafuatilia mafao akitumia jina langu, lakini walishikwa na hofu kutokana na mtu huyo kuwa na umri mdogo na kwa kumwangalia hajafika umri wa kustaafu, bahati nzuri ofisi ile inanifahamu," alisema.

Mzee huyo aliendelea kueleza kuwa alingiwa na hofu zaidi alipokumbuka kuwa mwaka 1989 akiwa Chuo cha Ualimu Mlutunguru, Ukerewe mkoani Mwanza, alilazimika kurejea nyumbani kumuuguza baba yake mzazi na aliporejea chuoni, alikuta jina lake limeshafanyiwa mtihani na mtu anayedaiwa anaishi Kahama.

Benedict aliishauri serikali kulinda maslahi ya wastaafu wanaofuatilia mafao yao ili kuwaepusha na utapeli unaofanywa na watumishi waliotumbuliwa kutokana na kuwa na vyeti feki au kutumia vyeti vya watu wengine.

Ofisa Elimu (Shule za Msingi) Halmashauri ya Mji wa Kahama, Aluko Lukolela, alidai ofisi yake haijapokea malalamiko ya aina hiyo na kuwatoa wasiwasi wastaafu kuwa kuna nyaraka za kujitosheleza tangu wastaafu walipoajiriwa na si rahisi mafao yao kutolewa kwa mtu asiyestahili.

Aliongeza kuwa kama mtumishi amesimamishwa kazi kutokana na kuwa na vyeti feki, hawezi kupatiwa mafao.

Kwa walimu ambao wamesimamishwa kazi kutokana na taratibu zingine za kiutumishi, Lukolela alisema watapatiwa stahiki zake kupitia chombo ambacho kinasimamia haki za walimu nchini.

# Chadema yalia rafu uchaguzi mitaa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimelalamikia kuhusu kile wanachokiita kukiukwa kwa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kunaodaiwa kufanyika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha wagombea wao kutokupewa fomu za kugombea au kupewa fomu pungufu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alidai yapo baadhi ya maeneo nchini ambayo wasimamizi wa uchaguzi huo wamekiuka kanuni za uchaguzi kwa kutokuwapa wagombea wa chama hicho fomu za kugombea kwa wakati licha ya wagombea wao kufika vituoni mapema.

"Kuna mambo sita makubwa ambayo tumeyabaini mpaka hatua ya sasa katika uchaguzi huu ambayo hayana afya kwa demokrasia ya nchi yetu," alidai Mrema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kuna baadhi ya maeneo yakiwamo majimbo la Vwawa mkoani Songwe na Mbozi mkoani Mbeya ambayo wagombea wa chama hicho walikuwa hawajapatiwa fomu za kugombea mpaka kufikia saa saba mchana huku ofisi za serikali za mitaa katika maeneo hayo zikidaiwa kufungwa.

Mrema pia alidai kuwa katika baadhi ya maeneo, wagombea wa Chadema wamekuwa wakipewa fomu pungufu kinyume cha kanuni, akifafanua kuwa mgombea anapaswa kupewa fomu tatu ikiwamo maadili.

Alidai kuwa baadhi ya maeneo nchini, fomu hizo hazijafika hivyo fomu wanapewa wagombea kuwa na upungufu wa kikanuni.

Chama hicho pia kimedai kuwa baadhi ya fomu wanazopewa wagombea wake zimerudufiwa na nyingine kutogongwa mhuri wa halmashauri, kitu ambacho Mrema alidai ni mkakati wa makusudi ili wagombea wao wawekewe pingamizi baadaye.

Jambo lingine ambalo limelalamikiwa na chama hicho ni kutokuwapo kwa waangalizi wa ndani wa uchaguzi huo.

Distributed via ippmedia






# Mshtakiwa kesi vigogo wa Nida ajisalimisha kwa DPP

**Na Hellen Mwango**

XAVERY Silverius, anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ameandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kuomba kukiri kuhujumu na kuomba msamaha.

Silverius na wenzake wanne akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Dickson Maimu, wanakabiliwa na mashtaka 55 likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Wakili wa Utetezi, Tully Kaundime, jana alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa juzi, lakini upande wa utetezi ulidai una hoja ya kuwasilisha.

Kaundime alidai kuwa mteja wake aliandika barua hiyo Septemba 26, mwaka

INAENDELEA UK.8

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuanze sasa udhibiti mbegu, pembejeo feki

**MVUA** zinazoendelea kunyesha licha ya kusababisha mafuriko kwenye maeneo mengine, ni fursa nyingine ya uhakika kwenye kilimo kwa sababu zimewahi na kunyesha kwa wakati. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi mara nyingi mvua huchelewa, hunyesha kidogo na kwa miaka kadhaa mvua za vuli zimekuwa na changamoto nyingi kwani hazipatikani. Mwaka huu kama ambavyo Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imekuwa ikitangaza, imeujulisha umma kuwa mvua ni nyingi na zitaendelea kunyesha kwa muda mrefu.

Tunaomba furaha ya mvua hii isiwe chanzo cha umaskini miongoni mwa wakulima ambao wanajikuta wakiuziwa mbegu feki.

Licha ya kwamba kuna wakala wa kudhibiti ubora wa mbegu TOSCI ni jukumu la mamlaka zinazohusika kuingilia kati na kuhakikisha kuwa wananchi hawadhulumiwa na kuuziwa mbegu zisizoota. Ndiyo wakati ambao wakulima wanatarajia kuona kazi za wakala wa mbegu za kilimo (ASA) na TOSCI ukifanyakazi za kuwadhibiti wadanganyifu ambao mara nyingi husababisha hasara kwa wakulima.

Ni ukweli kuwa wakulima vijijini na mijini mara nyingi wamejikuta katika tatizo la kuuziwa mbegu feki ndiyo maana nasi tunazikumbusha mamlaka za kuzalisha na kudhibiti mbegu kufuatilia ili kuepusha usambazaji mbegu duni kwa wakulima unaofanywa na wafanyabiashara wasio waadilifu.

Tunazikumbusha taasisi hizi wajibu wa kufuatilia kwa sababu mara nyingi mwanzo wa mvua kama hizi ambazo zimenyesha pengine bila wakulima kujiandaa ndiyo wakati wa wafanyabiashara wasio waadilifu kuwauzia mbegu feki wakulima ambao wengi walikuwa hawajajitayarisha kwa kilimo. Lakini si mbegu tu na pembejeo nyingine kama mbolea na viuatilifu ambavyo kama vile mbegu zisizoota, hupewa mbolea ambayo hairutubishi mimea na kemikali ambazo hazitibu mazao wala kuua wadudu na visumbufu.

Pengine ASA na TOSCI haziwezi kufika kila mahali kwa wakati, lakini kuna vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) hivi viko kila kijiji na kila kata na hawa wanawafahamu wanachama wao, pia wanawajua wauza mbegu, mbolea na pembejeo. Vyama hivi vina wajibu wa kusaka na kudhibiti wababaishaji hao na kufikisha taarifa ASA na TOSCI ili kuwakamata wahusika na kudhibiti mazoea hayo yanayosababisha hasara kwa wakulima wetu kila mwaka.

Tunahimiza ushiriki wa AMCOS kwa sababu baadhi ya wafanyabiashara wanatumia elimu ndogo na uelewa mdogo wa wakulima katika kutambua iwe mbegu, mbolea, au viuatilifu na kuwauzia bidhaa duni na feki.

Tunawakumbusha kuwa ni vyema kuweka kambi za kitaalamu na za wadhibiti kukagua mara kwa mara hasa kipindi hiki ili wanaouza pembejeo hizo wadhibitiwe mara moja na kuadhibiwa. Tunashauri kazi kufanywa mapema ili kukabiliana na matokeo mabaya maana hakuna tija iwapo ukaguzi utafanyika na kuwabaini wahusika ambao tayari watakuwa wamewaumiza wananchi.

Ikumbukwe kuwa wakulima wanatumia gharama kubwa kuandaa mashamba, kununua mbegu, mbolea na viuatilifu na iwapo yote hayo yatakwamishwa na uuzaji wa pembejeo feki hakuna atakayesaidia kufidia wala kupunguza gharama hizo. Pengine tunaona kwamba umefika wakati wa kukomesha mwenendo huu kwa kuwafungulia mashtaka na kuhujumu uchumi watuhumiwa wa kuuza pembejeo feki ili kukomesha mazoea hayo yanayotishia hatima ya kilimo na ustawi wa wakulima wetu ambao wengi ni maskini.

Wakati mwingine kuna haja ya kuandaa sheria ya kuwabana wauzaji na wakulima kutumia mbegu za kisasa na watakaoshindwa kufanya hivyo kuadhibiwa ikiwa ni njia mojawapo ya kukomesha matumizi ya pembejeo na mbegu feki.

Tunaamini kuwa jitihada hizi zitasaidia kudhibiti kuuza mbegu na kupenyeza pembejeo feki zinazowaumia wakulima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Haya yakizingatiwa, uchaguzi serikali za mitaa ni mteremko

Na Sabato Kasika

**KIPENGA** kwa ajili ya uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kilipulizwa jana, huku kukiwa na maelekezo ya kuzingatia kanuni za uchukuaji wa fomu hizo.

Uchukuaji na urejeshwaji wa fomu hizo unafanyika ndani ya siku saba na kufuatiwa na kampeni za uchaguzi zitakazodumu kwa muda wa siku saba na kisha uchaguzi kufanyika Novemba 24 mwaka huu.

Kampeni hizo zitatarajia kuanza Novemba 17 na kuhitimishwa Novemba 23 zikiwa zimefanyika kwa muda wa siku saba, ambao serikali inaamini unatosha kwa ajili ya uchaguzi huo.

Pamoja na kipenga kupulizwa, wadau wa uchaguzi, wakiwamo wagombea na vyama vyao, wamepewa maelekezo ya kuzingatia kwa lengo la kufanikisha mchakato huo.

Baadhi ya maelekezo hayo yaliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ni lile linalowataka wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha utoaji fomu hauingiliwi na changamoto ya aina yeyote.

Wasimamizi pia wanatakiwa kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake stahili ya kidemokrasia kama, ambavyo serikali inakusudia, ili kila mtu ashiriki katika uchaguzi huu bila kukwazwa na jambo lolote.

Kwamba ni muhimu kusimamia kanuni katika mchakato mzima wa kuchukua na kurejesha fomu.

Katika mwendelezo wa maelekezo hayo, hairuhusiwi kufanya kampeni kabla ya siku iliyoanishwa na kwamba hata kama kuna mbwembwe wakati wa kuchukua fomu au kurejesha, zisiwe katika mtindo wa kampeni.

Vyama vya siasa navyo vinatakiwa kuhakikisha vinatumia vizuri demokrasia kwa kupeleka watu wanaowakusudia na kuwadhamini kwa mujibu wa kanuni, huku watendaji wa vijiji na mitaa wakiwa hawaruhusiwi kutekeleza jukumu lolote linalopaswa kuamuliwa kwanza na halmashauri za vijiji au mitaa.

Muungwana anaamini kwamba iwapo maelekezo hayo ya serikali yatazingatiwa na vyama vya siasa, hakutakuwa na malalamiko ambayo yamewahi kujitokeza kwenye chaguzi zilizotangulia.

Wagombea na vyama vyao, wasimamizi na wadau wengine wazingatie kile ambacho kimeelekezwa na serikali, ili Watanzania washiriki katika uchaguzi huo.

Hapa si kuchagua tu bali wawe huru kuchagua viongozi wanaowataka, na ndiyo maana wasimamizi wanatakiwa kusimamia demokrasia, ili kila mtu apate haki yake stahili ya kidemokrasia kama, ambavyo serikali inakusudia.

Hivyo kwa muda wa siku saba, ambazo zimewekwa kwa ajili ya mchakato wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu, ni muhimu wagombea na vyama vyao kuzitumia vizuri kwa ustawi wa demokrasia nchini.

Malekezo hayo yakizingatiwa yatakuwa yamezima malalamiko ambayo yamewahi kuripotiwa na vyombo vya habari kuhusu wagombea kuwekeana mapingamizi kwa lengo la kukomoana.

Aidha, maelekezo hayo yanaweza kuondoa vilevile malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagombea kudai kuzuiwa kuchukua fomu au fomu zao kutopokelewa na wasimamizi.

Kwa maana hiyo Watanzania wanaotaka kushika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye serikali za mitaa, huu ndiyo wakati wao, lakini pia wazingatie maelekezo ya serikali.

Serikali inasema, katika uchaguzi huo hakutarajiwi kutokee changamoto ya aina yeyote, kwa vile jambo ambalo lilikuwa halijaeleweka vizuri, watu waliomba ufafanuzi na wakawa wamepewa.

Matarajio ya serikali ni kutaka wagombea wote wapatikane kwa haki kwa kuzingatia maelekezo ambayo imetoa kwa wadau wote wa uchaguzi.

Kuanzia wenyeviti wa vitongoji, katika mamlaka za miji midogo, mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa (kundi mchanganyiko la wanawake na wanaume) na wajumbe wa kamati ya mtaa (kundi la wanawake) katika mamlaka za miji wanapatikana kwa haki.

Maelekezo hayo hayahusu wagombea hao tu bali hata wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa halmashauri za vijiji (kundi mchanganyiko la wanawake na wanaume), wajumbe wa halmashauri za vijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya.

TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2019
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 9,197 | 12,455 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,893 | 12,491 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 25,470 | 22,920 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 104 | 384 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 122 | 112 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 91,576 | 89,971 |
| 12 | Mali Nyingine | 13,890 | 14,467 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,766 | 3,079 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **153,037** | **155,899** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,924 | 1,167 |
| 18 | Amana za Wateja | 109,315 | 110,887 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 3 | 23 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,519 | 4,122 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 12 | 15 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,171 | 1,173 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,239 | 1,182 |
| 28 | Madeni | 13,001 | 15,023 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **131,183** | **133,591** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **21,853** | **22,308** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,607 | 8,607 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,549 | 7,400 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 496 | 371 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 5,202 | 5,930 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **21,853** | **22,308** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 280 | 490 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 19,848 | 21,313 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 12,274 | 14,849 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1,459 | 1,459 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14.3% | 14.3% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 18.9% | 20.1% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 92.3% | 92.8% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 68.7% | 68.0% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 76.5% | 72.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.7% | -1.2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.8% | 4.5% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2019
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-19 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 7,289 | 6,807 | 21,494 | 21,773 |
| 2 Gharama za Riba | -1,416 | -1,162 | -3,895 | -4,235 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,873** | **5,645** | **17,600** | **17,538** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -795 | 933 | -1,403 | -3,156 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,412** | **2,469** | **5,180** | **6,366** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 95 | 18 | 252 | 74 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,010 | 1,889 | 3,978 | 5,283 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 307 | 561 | 950 | 1,009 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **-6,312** | **-8,205** | **-20,668** | **-24,912** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | -3,206 | -3,736 | -10,542 | -11,234 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | -3,106 | -4,468 | -10,126 | -13,678 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **178** | **843** | **708** | **-4,163** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | -53 | 0 | -212 | 0 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **124** | **843** | **496** | **-4,163** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **124** | **843** | **496** | **-4,163** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 433 | 450 | 433 | 450 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 14 | 98 | 58 | -484 |
| **15 Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.3% | 2% | 0.4% | -4% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.3% | 16% | 3.0% | -27% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 86.6% | 101% | 90.7% | 104% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 20.4% | 20% | 20.4% | 21% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **21,902,272** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 495,717 | 0 | 0 | 495,717 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (777,418) | 232,616 | 0 | (544,803) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 779,217 | 0 | (779,217) | - |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **8,044,260** | **2,769,873** | **-** | **21,853,186** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **8,607,136** | **2,431,917** | **12,981,019** | **694,193** | **843,314** | **25,557,579** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | -4,163,274 | 0 | 0 | -4,163,274 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | -2,266,432 | 2,234,954 | 0 | -31,478 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 101,631 | 0 | -101,631 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2018** | **8,607,136** | **2,431,917** | **6,652,944** | **2,929,147** | **741,683** | **21,362,826** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.09.2019
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 178 | 313 | 708 | -2,202 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Hasara Katika Mali | 339 | 383 | 1,139 | 397 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | -1,605 | -7,347 | -8,580 | 3,844 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | 4 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | -874 | -1,304 | -7,578 | -7,900 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | -2,255 | -3,205 | 1,395 | 1,235 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | -1,780 | 7,759 | 5,085 | 2,031 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | -211 | -373 | -1,137 | -1,153 |
| | - Kodi Iliyolipwa | 0 | 144 | 0 | 0 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 1,165 | 321 | 1,543 | 769 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **-5,044** | **-3,310** | **-7,424** | **-2,975** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 79 | -320 | -427 | -158 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 3 | 0 | 3 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **82** | **-320** | **-424** | **-158** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | -4,962 | -3,630 | -7,849 | -3,133 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 16,698 | 20,327 | 19,584 | 21,001 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **11,735** | **16,698** | **11,735** | **17,868** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2019

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

***Jina na Cheo*** ***Saini*** ***Tarehe***

Augustine Akowuah
**(Mtendaji Mkuu)**

Bertha Simon
**(Mkuu wa Fedha)**

Chemo Mutani
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

***Jina*** ***Saini*** ***Tarehe***

1. Ernest Massawe

2. Dr. Josephat Daniel Lotto




Distributed via ippmedia

## HABARI KITAIFA

# Taboa yafunguka kukatika kwa mawasiliano Kaskazini


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **UNITED BANK FOR AFRICA,** tutauza kwa MNADA WA HADHARA, dhamana ya mkopo wa mdaiwa wao ambayo ni NYUMBA YA MAKAZI. Mnada utafanyika siku ya jumamosi tarehe 29/11/2019 saa 4:00 asubuhi. Mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini.

| s/n | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | MKINDO GENERAL MOTORS | NYUMBA YA MAKAZI YENYE HATI NA. 106380, ILIYOPO KIWANJA NA. 2630, KITALU "A". ILIYOPO ENEO LA KIMARA MATANGINI, MANISPAA YA UBUNGO. ILIYOPO KWA JINA LA VITUS MWALIKANGIME MBILIGI. | 29/11/2019 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji,
UBA Bank,
30C/30D Nyerere Road,
P.O Box 80514,
DAR ES SALAAM.
Tel: +255 2863452/3
Fax: 2863254

214643102


**Na Salome Kitomari**



SIKU chache baada ya Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), kusema mawasiliano ya wilaya ya Handeni mkoani Tanga yatarejea ndani ya siku tatu, Chama cha Wasafirishaji Tanzania (Taboa), kimefunguka.

Taboa imeitaka serikali kutafuta suluhisho la kudumu la madaraja ya Mkoa wa Tanga ambayo nyakati za mvua nyingi huzolewa na mvua.

Akizungumza jana na Nipashe, Katibu wa Taboa, Enea Mrutu (pichani), alisema daraja la Mandera linapaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee na hatua ya kuimarisha miundombinu kuchukuliwa.

"Nakumbuka tangu nikiwa dereva miaka ya 70 hadi 88, eneo hilo ni korofi kwa nyakati za mvua, kuna wakati basi lilisombwa na maji na kusababisha vifo vya watu wengi," alisema.

Aidha, alisema wataalamu wa miundombinu wanafahamu eneo hilo, na kwamba si mara ya kwanza hali kuwa hivyo, na imekuwa ikijirudia kila kunapokuwa na mvua nyingi.

"Ifike wakati serikali ijenge upya miundombinu ya eneo hilo wasijenge kwa kufuata barabara ilivyoteremka, bali wanyanyue daraja liwe juu kwa kuwa ni eneo korofi linalojulikana," alisema Mrutu.

Alisema kutokana na mvua za hivi karibuni wasafirishaji na wasafiri wameishi katika wakati mgumu ikiwamo kuongeza gharama za matumizi ambayo hawakuyatarajia.

"Magari yamekaa siku mbili eneo hilo, wapo ambao walilazimika kupitia njia nyingine kwenda hadi Dodoma ndipo wafike mikoa ya Kaskazini na wengine kurudi walikotoka, kwa ujumla iliongeza gharama za uendeshaji na usumbufu," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema kazi inayoendelea kwenye maeneo ambayo wanaimarisha kingo zilizobomoka, alafu ndiyo watandaze madaraja ya muda yanayotumiwa na jeshi

Alisema wakishamaliza kujenga kingo watapachika madaraja, lakini kazi kubwa inayofanywa sasa ni ujenzi wa kingo imara ili madaraja yasibebwe.

Naye Meneja wa Tanroads, mkoa wa Tanga, Mhandisi Alfred Ndumbaro, alisema kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi (JWTZ), wamerejesha mawasiliano kwenye barabara mbalimbali, huku wakiendelea kuimarisha miundombinu kwenye maeneo yenye uharibifu mkubwa.

Distributed via ippmedia




## Mshtakiwa kesi vigogo wa Nida ajisalimisha kwa DPP

**INATOKA UK. 3**

huu, lakini mpaka juzi walikuwa hawajapewa majibu kuhusiana na maombi hayo.

Kutokana na hali hiyo, wakili huyo aliomba upande wa mashtaka ueleze umefika hatua gani baada ya mteja wake kuwasilisha barua kwa DPP.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini Jamhuri inaomba kuwabadilishia washtakiwa hati ya mashtaka kwa kumwondoa mshtakiwa Astery Ndege. Mahakama hiyo ilimhukumu Ndege kulipa fidia ya Sh. 293,446,400.23 baada ya kuandika barua ya kukiri makosa yake ya kutakatisha fedha.

Ndege ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, alilipa fidia hiyo ikiwa ni sehemu ya hasara iinayodaiwa kusababishwa na washtakiwa hao ya Sh. bilioni 1.175.

Hakimu Ally baada ya kusikiliza hoja za pande zote, aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 11, mwaka huu itakapokuja kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali. Mbali na Maimu, washtakiwa wengine katika hati mpya ya mashtaka ni Avelin Momburi, George Ntalima, Xavery Silverius, maarufu kama Silverius Kayombo, na Sabrina Raymond.

Katika kesi hiyo, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 55 yakiwamo ya kuongoza genge la uhalifu, kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

## Ujenzi barabara za mzunguko waanza

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imezindua rasmi ujenzi wa barabara za mzunguko za njia nne za urefu wa kilomita 112.3 jijini Dodoma ambazo ujenzi wake unagharimu kiasi cha Sh. bilioni 494. Fedha hizo zimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ADB Sh. bilion 412, ambapo ni sawa na asilimia 83.4, huku serikali ikitoa Sh. billion 82 sawa asimia 16.6.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema huo ni mpango mkakati wa serikali wa kupunguza msongamano katika Jijini la Dodoma kutokana na kuwa na ushoroba mkali wa barabara kuu inayotoka Cape Town (Afrika Kusini) hadi Cairo (Misri), hivyo kutakuwa na msongamano mkubwa wa magari. Alisema Sh. bilioni 17 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia mali ambazo zitaathiriwa kwa wananchi walengwa watakao pitiwa na ujenzi wa mradi huo. Alisema kuwa mradi huo ni mkubwa ambao utaenda sambamba na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato ambapo baada ya serikali kupokea ndege mpya pili itaanzisha safari ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mhandisi Patrick Mfugale, alisema mradi huo utakuwa ni wa kilomita 112 .3 ambapo zitajengwa barabara za mzunguko kilomita 15 kila upande kabla ya kuingia jijini Dodoma.

Alisema kutakuwa na miradi mingine midogo, ambapo watajenga vituo vya afya vitano katika vijiji vya Mahomanyika, Vyeyula, Nala, Ihumwa pamoja na Matumburu pamoja na kutoa magari ya kubebea wagonjwa.

Alisema pia watakarabati Shule ya Msingi Chiwanga pamoja na uchimbaji visima virefu vyenye urefu wa mita 200.

Mfugale alisema watakarabati barabara chache za jijini hapa ambazo ni kilomita 28.3 ambazo ni kutoka Kizota hadi Zuzu.

## HABARI KITAIFA



Mafundi wa Kampuni ya Yapi Merkezi wanaojenga reli ya treni ya mwendokasi ya kisasa, wakiendelea na ujenzi wa barabara ya juu maeneo ya Gerezani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wabunge walivyoibana TPA mfumo wa Tehama

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeibana Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa kushindwa kufunga mfumo thabiti wa Tehama na kudai kuisababishia hasara serikali kutokana na makusanyo ya mapato kidogo.

Hali hiyo ilijitokeza juzi wakati kamati hiyo ikifanya mahojiano na TPA kufuatia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka ulioishia Juni 2018.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema kamati yake imesikitishwa na utendaji kazi wa TPA kutokana na kushindwa kutekeleza agizo la kusimika mfumo huo kwa muda mrefu.

Kaboyoka alisema mamlaka hiyo inategemewa kwa kiasi kikubwa na serikali kukusanya fedha, lakini kama mifumo haifanyi kazi haitaweza kutekeleza jukumu hilo.

"Rais wetu amekuwa akizungumzia mara kadhaa kuhusu upotevu wa fedha katika mamlaka hii...Kamati hii haitatoa maagizo tena kwa mamlaka hii kuhusu usimikaji wa mfumo kwa kuwa kwa miaka mitatu mfululizo tumeagiza bila ya utekelezaji," alisema.

Aliongeza: "Tutakaa baadaye na kujua hatua tutakayochukua na kutoa mapendekezo kwa mamlaka ya uteuzi, kwa sababu hata tukitoa maagizo hadi auditing ifanyike mwakani yatakuwa mambo haya haya."

Mwenyekiti huyo alisema: "Ni fedha kiasi gani inapotea wakati mfumo haufanyi kazi. Rais anategemea hili shirika kuleta fedha za kuendesha nchi."

Awali, akichangia Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, alisema kamati hiyo ilitoa agizo kwa TPA, msajili na kampuni iliyopewa kandarasi hiyo ya kufunga mfumo huo kukutana ili kuhakikisha mfumo huo unafungwa. Alisema kandarasi hiyo ilikuwa imefanya kazi takribani karibu robo tatu ya kazi na fedha nyingi zimelipwa, lakini menejimenti ya TPA ilipofika kwenye kamati walisema wanataka apatikane mtu mwingine.

Kigua alibainisha kutokuwapo kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya bandari kumeifanya Mamlaka ya Mapato (TRA) ifanye kazi hiyo kwa muda wakati jukumu hilo linapaswa kufanywa na TPA.

"Ukiangalia taarifa ya CAG, maelekezo ya kamati yako wakutane na mkandarasi halijatekelezwa na tafsiri yake ni kuwa kamati yako

INAENDELEA UK. 10

## Wenye ualbino wapewa elimu

**Na Ndalike Sonda**, KAHAMA

KATIKA kukabiliana na changamoto za unyanyasaji dhidi ya watu wenye ualbino, Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kimeanza kutoa elimu shuleni ili kuwajengea uelewa wanafunzi namna ya kuwaona watu wenye ualbino ni kama watu wengine.

Katibu wa TAS, Wilaya ya Kahama, Sitta Masenya, akizungumza kwenye kijiji cha Masabi, alisema bado changamoto za unyanyapaa zipo katika jamii, hivyo ni lazima elimu itolewe ili kukabiliana na changamoto hiyo, huku akiiomba serikali kuendelea kuimarisha ulinzi kwa watu wenye ualbino.

Alisema wameamua kuanzia kwenye shule kwa kuwa huko kuna kundi kubwa la watoto ambao wakifundishwa watakuwa mabalozi wazuri katika jamii, na kwamba elimu hiyo pia wanaitoka katika ngazi ya vijiji na kata.

Naye Mwenyekiti wa TAS, wilayani humo, Ngassa Mrisho, alisema watu wenye ualbino ni watu kama wengine wenye uwezo wa kushiriki katika shughuli zote za kijamii hivyo ni vyema wakashirikishwa kuanzia ngazi ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Miongoni mwa wanafunzi waliopatiwa elimu hiyo ni kutoka katika Shule ya Msingi Masabi Kata ya Mega katika Halmashauri ya Msalala, ambapo baadhi ya wanafunzi wamepata elimu ya kutosha juu ya kuwapenda watu wenye ualbino na kuahidi kushirikiana nao katika masomo na shughuli zingine.

# Sababu shule za serikali D'Salaam kutofanya vizuri

**Na Daniel Limbe**

ZIKIWA zimesalia siku saba kuanza mitihani ya kuhitimu kidato cha nne mwaka 2019, baadhi ya wadau wa elimu wameeleza sababu za shule nyingi za serikali jijini Dar es Salaam kufanya vibaya kwenye matokeo.

Wamedai iwapo changamoto zilizopo zikifanyiwa kazi kwa kuunganisha nguvu kati ya serikali, wadau, walimu, wazazi na wanafunzi hakika mapinduzi makubwa ya kielimu yatapatikana ukilinganisha na hali ilivyo sasa.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiluvya Kata ya Kibamba Manispaa ya Ubungo jijini Da es Salaam, Christina Mwita, amedai licha ya shule yake kufanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha pili na nne kwa shule za umma, bado shule nyingi zinakabiliwa na uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Akitoa mfano kwa shule hiyo licha ya kuwa na wanafunzi 1,465 wavulana wakiwa 700 na wasichana 765, alisema kuna uhaba wa jengo la maktaba, jengo la utawala, kompyuta, makabati, meza pamoja na viti ambapo wanalazimika kutumia vya wanafunzi kwa lengo la kuandikia na kukalia.

Changamoto nyingine ni kukosekana kwa uzio hali inayosababisha baadhi ya wananchi kuharibu miundombinu ya shule pamoja na wanafunzi kutoroka shuleni na kujiunga kwenye makundi ya kihalifu.

Hatua hiyo husababisha wanafunzi kutumia dawa za kulevya, uhalifu na kufanya ukahaba, hali ambayo imedaiwa kuwa chanzo cha kuporomoka kwa ufaulu kwa baadhi ya wanafunzi wa sekondari jijini Dar es Salaam.

Mwalimu Christina alikuwa kwenye mahafali ya wanafunzi wa kidato cha nne wa Kiluvya Sekondari wanaotazamiwa kuhitimu mwaka huu.

Hata hivyo, Dk. Kessy Kopwe, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alilieleza Nipashe siri ya mafanikio kwa wanafunzi kufikia ndoto zao kwamba ni kujiwekea malengo mazuri.

Kadhalika, kuwa na nidhamu kwa wazazi, walimu na jamii, kutumia muda wao vizuri kwa kutenda mambo mema yawapasayo, kuwa na vipaumbele, kutafuta maarifa nje ya darasa na kuchagua marafiki bora.

Moja wa wanafunzi wa kidato cha nne wa shule hiyo, Kenned Songolo, mbali na kuipongeza serikali kwa kutoa elimu bure, aliwasisitiza wazazi kuthamini vipaji vya watoto wao pamoja na kushirikiana na serikali kuhakikisha watoto wote wanapata elimu bora kwa kuwatimizia mahitaji yao.

Magwaiga Magesa, mkazi wa Kiluvya, alisema kutofanya vizuri kwa shule za umma inatokana na baadhi ya wazazi na jamii kushindwa kutimiza majukumu yao katika malezi ya watoto, na kwamba kuna haja kubwa ya kutambua kuwa viongozi bora wa kesho huandaliwa mapema.

## Wabunge walivyoibana TPA mfumo wa Tehama

INATOKA UK. 9

mwenyekiti inadharauliwa," alisema.

Kuhusu hoja ya ardhi iliyonunuliwa Ihumwa jijini Dodoma, alisema TPA iliamua kulipa Sh. bilioni 6.3 bila kufuata utaratibu wa manunuzi wa serikali.

"CAG amethibitisha malipo ya eneo hilo yalifanyika kwa barua na malipo hayo yalikuwa yafanyike kwa awamu tatu yaani asilimia 40, asilimia 40 na kumalizia asilimia 20, lakini wao walilipa asilimia 50 ya malipo yote kinyume cha utaratibu," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa CAG tathmini ilifanyika Mei 20, mwaka 2019, takribani miaka mitatu ya baada ya malipo wakati wao walitakiwa kufanya tathmini kabla ya kulipa.

Naye Mbunge wa Ole (CUF), Juma Hamad Omar, alisema kutokana na kutokuwa na mfumo makusanyo ya madeni ya TPA yamepanda kwa miaka mitatu.

Alieleza kuwa madeni hayo yamepanda kutoka Sh. bilioni 106.4 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2016 hadi kufikia Sh. bilioni 458.5 kwa mwaka unaoishia Juni 2017, huku mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2018 yamefikia Sh. bilioni 701.6.

"Kutokusanywa kwa madeni hayo kumeathiri pia faida ya mamlaka hiyo ambayo imepungua kutoka Sh. bilioni 78.6 Juni 30 mwaka 2017 hadi kufikia Sh. bilioni 68.5 Juni 2018, nisingetarajia shirika hili linatangaza faida ya Sh. bilioni 68.5, mamlaka imekuwa kaidi," alisema.

Akijibu hoja za wajumbe hao, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Prof. Ignas Rubaratuka, alifafanua kuwa kampuni TTCS iliyopewa kandarasi ya kufunga mfumo chini ya leseni ya Kampuni ya ERP-SAP, lakini baada ya changamoto hiyo iliyotokea imekubali kukamilisha kazi iliyobaki kwa gharama ya chini ya asilimia 30.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema wataendelea kutekeleza maagizo ya kamati hiyo na kwamba suala la kusimika mfumo litakamilika.

"Msajili wa Hazina aliunda kamati mara baada ya maagizo ya Bunge ambayo ilikabidhiwa nyaraka zote stahili za mradi huo," alisema.

Kuhusu ardhi ya Ihumwa, Mkurugenzi huyo alisema walikwenda kuchukua ardhi kwa mwenye mamlaka ambaye ni iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (CDA) iliyokuwa na utaratibu wake wa kufuatwa.

# 797 wafundishwa kilimo kinachohimili tabianchi

**Na Beatrice Philemon**

JUMLA ya wakulima 797 katika mikoa minne wamepata mafunzo juu ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi ili kukabiliana na athari za mabadiliko hayo, kuongeza tija, kipato na kurutubisha udongo.

Akizungumza na Nipashe baada ya mafunzo ya uhamasishaji wa wanahabari kuhusu kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na lishe, ofisa kilimo wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Kilimo cha Kitropiki (IITA), Sigismund Mujuni, alisema mafunzo hayo yalitolewa bure kwa wakulima katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 na 2018/2019.

Alisema mafunzo hayo yalitolewa katika mkoa wa Dodoma, Morogoro, Lindi, Iringa katika Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Mvomero, Ruangwa na Dodoma.

Kupitia Mradi wa Kujenga uwezo katika Kilimo Himilivu kwa mabadiliko ya Tabianchi, (BCRFS) unaofadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), wakulima walifundishwa teknolojia mbalimbali ambazo zitawasaidia kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi. "Walifundishwa jinsi ya kutumia teknolojia ya Tie-ridging (matuta ya kufunga), jinsi ya kuchanganya mimea jamii ya mikunde kunde na mazao mengine (intercropping,) chololo pits, teknolojia ya matuta ya fanya juu na fanya chini ikiwamo kutumia mbegu bora zinazovumilia ukame," alisema.

Pia walifundishwa teknolojia ya kuvuna maji shambani, kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuhifadhi unyevu nyevu shambani.

Mbali na hilo, IITA iliandaa mashamba darasa katika kila kijiji ambapo wakulima walipata mafunzo ili waweze kuona na kuchagua teknolojia inayowafaa katika kuhimili mabadiliko ya tabia nchi.

Lengo la mafunzo hayo ilikuwa ni kuwajengea uwezo ili wawe na ujuzi ambao utawasaidia kuweza kutumia teknolojia hizo katika shughuli zao za kilimo ili kuongeza tija, kipato.

Kati ya hao, wakulima 358 walipata mafunzo katika kijiji cha Hombolo na Nghumbi katika mkoa wa Dodoma katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 and 2018/2019.

Katika Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, wakulima 154 walipata mafunzo katika kijiji cha Image na Mtandika kwa msimu wa kilimo wa 2018/2019.

Pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, wakulima 156 walipata mafunzo katika kijiji cha Kimambira na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Ilonga (MATI) katika msimu wa kilimo wa mwaka 2018/2019.

Katika Wilaya ya Ruangwa, jumla ya wakulima 129 walipata mafunzo katika kijiji cha Chienjele and Machamaja katika msimu wa kilimo wa mwaka 2018/2019.

Alisema katika kijiji cha Mtandika na Image, Wilaya ya Kilolo IITA ilifundisha wakulima teknolojia ya matuta ya fanya juu na fanya chini, jinsi ya kutumia mbegu bora za mahindi, maharage na alizeti na walichanganya mahindi na maharage na walionyesha namna bora za kuchanganya haya mazao yalete ufanisi.

Pia IITA imekuwa ikishiriki maonyesho ya Sanenane Dodoma kuonyesha hizi teknolojia ikiwamo kilimo himilivu (Climate Smart Agriculture).

Naye Ofisa Mawasiliano wa IITA, Catherine Njuguna, alisema katika utoaji wa mafunzo wanashirikiana na Wizara ya Kilimo na wadau wengine.

Alisema USAID ilitoa dola za Kimarekani milioni 2 kwa IITA ili kutekeleza mradi wa kujenga uwezo katika Kilimo Himilivu kwa Mabadiliko ya Tabianchi, (BCRFS) Tanzania Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Wilimo na wadau wengine.



Wafanyausafi wakitoa mchanga katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaaam jana, uliotokana na mvua zilizonyesha hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madiwani wanawake wafundwa

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, amewataka madiwani wanawake nchini kuzidisha upendo baina yao na kuacha unafiki, huku wakijifunza kukaa kimya, jambo litakalowasaidia kushika nafasi za uongozi kwenye kata zao na kukamilisha dhana ya serikali ya 50 kwa 50.

Kingo ambaye ni Diwani wa Ngerengere wilayani humo, alisema hayo jana wakati akizungumza na baadhi ya madiwani wanawake na wa Viti Maalum walioshiriki warsha ya siku tatu kwa wanawake watia nia ya kugombea uwenyeviti wa vijiji na vitongoji katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP- Mtandao).

Alisema, akiwa diwani kamili anaamini suala la upendo na kutokuwa na unafiki linaweza kumfanya kiongozi kuzidi kukua katika nyadhifa mbalimbali za uongozi. "Jifunze kukaa kimya na sio kila jambo unalosikia au kuliona unatakiwa uliseme, unatakiwa uangalie la kuongea na mahali la kuongea," alisema Kingo. Aidha, alisema Wilaya ya Morogoro ina jumla ya kata 31 za uchaguzi, na kwamba mpaka sasa wanawake wameshika kata 6 ambapo anatarajia katika uchaguzi ujao mwakani wanawake wataendelea kushika nafasi na kufikia hata kata 10 zenye madiwani wanawake.

Hata hivyo, aliwataka kutambua kuwa 50 kwa 50 haiji kwa kusubiriwa bali kwa kuidai na kuitafuta ambapo aliwataka kutokubali kubaguliwa ili kufikia lengo linalokusudiwa.

Hivyo aliwaasa madiwani ambao ni walezi wa kata kuendelea kuwa walezi wazuri kwa kata zao na watu wake kwani kufanya hivyo kutawaongezea imani wapigakura. Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Rehema Saidi Bwasi, aliwataka washiriki hao kwenda kuyatumia vyema mafunzo hayo waliyopewa ili kupata kushika nafasi mbalimbali za uongozi ambazo haziji bila ushirikiano kwa lengo la kupata usawa wa 50 kwa 50.

Awali mwezeshaji wa warsha hiyo kutoka TGNP, Dk. Consolata Sulley, alisema lengo la warsha hiyo ni kuwajengea uwezo wanawake wa wilaya hiyo waliotia nia katika kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Dk. Sulley ambaye ni Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema warsha hiyo pia imelenga kuwatoa hofu na kuwatia moyo sambamba na kuwafahamisha namna mchakato wa uchaguzi unavyotaka mtu kuwa na moyo wa ujasili tofauti na hali ilivyo mara nyingi mwanamke amekuwa akionekana kuwa muoga. Dk. Selley aliwataka wanawake waliotia nia kutambua kuwa mambo ya kuvunjana moyo yapo sehemu mbalimbali hata kwenye familia ambapo alisema mada juu ya jinsia na uchaguzi zinaeleza tofauti za kimajukumu juu ya mwanamke na mwanaume na kwamba mara nyingi katika wigo wa kisiasa inaamini kuwa kiongozi ni mwanaume na kumbe majukumu ya uongozi ni ya wote.

# Malengo 17 ya UN kupelekwa Mlima K'njaro

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

VIJANA mbalimbali kutoka nchi za Afrika, wamejipanga kupanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kuhamasisha wenzao kushiriki katika kutimiza Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDG) ya Umoja wa Mataifa (UN).

Aidha, vijana hao watakuwa wa kwanza kupeleka bango la malengo hayo katika kilele cha Mlima Kilimanjaro ili kila atakayefika kileleni aone na kukumbuka malengo hayo.

Mratibu wa Mpango huo, Munyaradzi Muzenda, kutoka Zimbabwe alisema jana kuwa wanaendesha kampeni ya Mlima Kilimanjaro isemayo 'Ishi Ndoto Zako' ambayo inalenga kuhamasisha malengo endelevu ya UN na kuhamasisha malengo ya Umoja wa Afrika 263 ya Afrika wanayoyataka.

"Ni vyema kila kijana akahakikisha anashiriki kutangaza malengo ya UN kwa kupanda Mlima Kilimanjaro na ili iwe hamasa kwa wengine," alisema.

Munyaradzi alisema vijana 17 watapanda na vibao vya malengo hayo, wakijikita zaidi kwenye lengo namba moja la kuondoa umaskini na kuhimiza vijana kushiriki katika shughuli zitakazosaidia kutokomeza umaskini.

Pia alisema Tanzania itakuwa nchi ya kwanza duniani kupeleka malengo hayo katika mlima huo wa pili kwa urefu duniani, hivyo amewataka wadau kuungana katika kampeni hiyo ya kupanda mlima mwishoni mwaka huu.

Vijana kutoka mataifa mbalimbali watafika Arusha, kwa ajili ya kupanda mlima na wanatarajia kupitia kampeni hiyo, watafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Aliongeza vijana ni kundi kubwa linalotegemewa katika nchi zote duniani, hivyo ni vyema



Meneja Masoko wa Kiwanda cha Maziwa cha Grande Demam, Japhet Mwahakila, akionyesha kwa waandishi wa habari, jinsi siagi inavyosindikwa kabla ya kwenda kwa mteja, walipofanya ziara kiwandani hapo, Usa River wilayani Arumeru, jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Babati kicheko fedha ukarabati shule

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imeishukuru serikali kwa kuipatia Sh. milioni 501 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari kwa miaka mitatu iliyopita. Shukrani hizo zilitolewa juzi na Mchumi wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba, alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Katimba alisema inawajali na kuthamini wananchi wote bila ubaguzi kwa kuwa inatoa fedha nyingi na bila kujali itikadi wala ukabila.

"Kweli tunamshukuru sana Rais (John Magufuli) kwa makubwa anayotutendea. Yaani serikali hii hakika ni ya wanyonge maana halimashauri yetu hatujawahi kupokea fedha kama hizi katika serikali zingine," alisema.

Alisema baada ya kupokea fedha hizo, walitoa Sh. milioni 395 kwa ajili ya kukarabati vyumba 35 vya madarasa ya sekondari na vyoo, huku Sh. milioni 152 zinatarajia kujenga mabweni mawili ya sekondari ya Nakwa. Katimba alisema kwa shule za msingi kwa mwaka 2018/19, zilitolewa Sh. milioni 106 kwa ajili ya kurekebisha mfumo wa takwimu na shughuli zingine.

Pia alisema serikali imejenga madarasa manne ambayo ni ya shule za msingi za Harambee. Osterbay Babati na Ziwani ambayo ujenzi wake uligharimu Sh. milioni 12.5. Alisema ili kuboresha miundombinu, serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa lengo la kuwezesha watoto wasome vizuri. "Tunaimani tunaboboresha miundombinu ya wanafunzi, tunawezesha wanafunzi au watoto wetu kusoma vizuri na kwa bidii kwa sababu mazingira ya elimu yanawaruhusu kujisomea kwa amani na utulivu," alisema.

# BAWASA yatoa ofa Maji kuvutia wateja

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya MajiSafi na usafi wa Mazingira Mjini Babati (Bawasa) imetoa punguzo la asilimia 20 kwa wateja wapya na wateja wenye madeni, ili kuhakikisha wananchi wote wanapata maji na kuwavutia wengi zaidi kupata huduma hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bawasa, Mhandisi Iddy Msuya, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake, kuhusu huduma ya utoaji maji safi kwa wananchi.

Alisema punguzo hilo wanalitoa kila wiki ya kwanza ya mwezi ili kuwafikia wananchi kiurahisi katika huduma yao na kufikia malengo ya serikali ya upatikanaji bora wa huduma ya maji, ifikapo mwakani.

Msuya alisema punguzo hilo la huduma kwa mteja linalenga wateja wapya ambao watapunguziwa asilimia 20 huku akitoa mfano kuwa kama gharama za vifaa vyote alitakiwa alipe Sh. 100,000 mteja anapunguziwa Sh. 20,000.

"Kwa wale wateja waliondolewa huduma kwa kushindwa kulipa billi zao tunarudisha maji bila kulipia ile faini ya Sh. 15,000. Mfano mteja alitakiwa alipe Sh. 20,000 akashindwa akakatiwa ukiweka na faini alitakiwa alipe Sh. 35,000 sasa atalipa Sh. 20,000 tu alizokuwa anadaiwa," alisema.

Alisema ofa hiyo inatakiwa iishie kesho lakini uongozi wa Bawasa unatarajia kukaa na Bodi ya Wakurugenzi na kuwaomba iendelee mpaka mwishoni mwa mwezi ujao.

Alifafanua kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Mji wa Babati na viunga vyake ni asilimia 82, hivyo wananchi waendelee kuiamini mamlaka hiyo kwa huduma wanayoitoa.

Licha mafanikio hayo. Alisema mamlaka inakabiliwa inakabiliwa na uhaba wa matangi kwa kuwa yaliyopo ni madogo, hivyo kushindwa kutoa huduma kwa urahisi pamoja na vyanzo vya maji kuvamiwa na wananchi.

Changamoto nyingine alisema ni wananchi kuiba maji na kwamba kwa mwaka huu wameshakamata wezi 15 ambao wametozwa faini na wengine wamekubaliana nao wawe wanalipa kidogo kidogo.

Distributed via ippmedia

## Wazazi wakumbushwa umuhimu lishe watoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** MOSHI

WANANCHI wa Wilaya ya Moshi wametakiwa kushiriki katika vita dhidi ya udumavu miongoni mwa watoto kwa kulima mboga na matunda na kuvitumia vizuri ili kuhakikisha kuwa watoto hawapati tatizo hilo na hatimaye kukua vizuri kimwili na kiakili.

Mratibu wa Mradi wa Lishe unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Initiative for Youth , Laurent Sabuni, alisema hayo jana alipotembelea klabu za lishe zilizoundwa shuleni katika wilaya hiyo ambayo imelenga kuhamasisha ulimaji wa bustani za mboga na kutumia mboga kwa wingi pamoja na vitamin ili kuondokana na tatizo la lishe duni.

Sabuni alisema wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo la udumavu kwa watoto licha ya wazazi wao kuwa wakulima wazuri wa mboga na matunda ambayo mara nyingi wanauza na kupata fedha.

"Tunafanya kampeni ya lishe katika kata sita za Wilaya ya Moshi ambazo ni Mabogini, Matala, Masaera, Kilimaposo na Makuyuni huko tunafika katika vijiji kuelimisha juu ya namna ya kuandaa lishe bora kwa familia na watoto. Pia tumeunda klabu za lishe shuleni ambazo tunatoa elimu kwa kushirikiana na maofisa lishe ili kutokomeza tatizo la udumavu," alisema Sabuni.

Hata hivyo, Sabuni alifafanua kuwa ushirikishwaji wa wananchi umekuwa ukifanyika kwa kuwafikia wananchi kupitia mikutano ya vijiji na kutembelea kaya kwa kaya hususan ambazo ziko hatarini kupata udumavu ili kuwanusuru.

Mtaalamu wa Lishe kutoka shirika hilo, Elias Joel, alisema kuwa wamekua wakitoa elimu juu ya uandaaji wa mboga na matunda ili yasipoteze virutubisho muhimu vinavyohitajika kwenye mwili juhudi ambazo tayari zimeanza kuzaa matunda kwa wananchi hususan kinamama wameanza kuwa na mwamko juu ya namna ya kuandaa lishe bora hivyo tunawashukuru wafadhili wa mradi ambao ni Shirika la Global Alliance for Improved Nutrion Gain kwa kutuwezesha kuwafikia wananchi na kupata matokeo mazuri.

# Miradi ya ujenzi kufanyiwa tathmini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MIRADI yote ya umma inayojengwa kwa fedha za serikali katika Mkoa wa Kilimanjaro itafanyiwa tathmini upya, baada ya amri ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa tathmini hiyo ni miongoni mwa maelekezo yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, wiki iliyopita.

Mabula ameagiza kufanyika kwa tathmini ya miradi yote ya ujenzi inayoendelea mkoani hapa ili kuhakikisha vifaa vya ujenzi vinavyotumika vinakidhi viwango vinavyohitajika kisheria.

"Nimeagiza baada ya kutembelea miradi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika wilaya za Hai na Rombo. Nimeridhika na uamuzi wa NHC kununua vifaa nje ya Kilimanjaro ili kuendana na agizo la serikali la kuhakikisha vinatumika vifaa vyenye kukidhi viwango. Uamuzi huu ni wa kuungwa mkono maana ni matumizi mazuri ya kodi za wananchi," alisema Mabula juzi alipoulizwa kuhusu agizo hilo.

Nipashe ilizungumza pia na Kaimu Meneja wa NHC Mkoa wa Kilimanjaro, Stanley Msofe, ambaye alisema katika Wilaya ya Hai wanaendelea na mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai ambalo litagharimu Sh. 910, 585, 940 hadi utakapokamilika.

Aliutaja mradi mwingine ni ujenzi wa ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) eneo la Rongai, Rombo na nyumba tatu za watumishi wa taasisi hiyo wilayani humo.

"Mradi utagharimu Sh. 532,924,819.05 na unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi 10 kuanzia Septemba, mwaka huu," alisema.

Akizungumzia changamoto zinaoukabili mrdai huo wa Rombo, Msofe alisema ni pamoja na baadhi ya malighafi zinatumika kuagizwa kutoka nje ya Wilaya ya Rombo na nyingine nje ya Mkoa wa Kilimanjaro.

"Mchanga tunatoa wilayani Mwanga kutokana na huu ulioko hapa kutokuwa mzuri kwa ujenzi na chuma tunaagiza kutoka Dar es Salaam maana vinavyopatikana hapa Kilimanjaro havikidhi viwango vinavyohitajika katika kutekeleza miradi ya ujenzi ya serikali," alisema.

Awali, Meneja Mawasiliano wa NHC, Muungano Saguya, alitoa wito kwa taasisi za serikali na zile za binafsi kulitumia shirika hilo katika kutekeleza miradi ya ujenzi.

"Tayari shirika letu lina leseni ya ujenzi Daraja la Kwanza na pia tuna miradi mingi ikiwamo ile ya serikali ambayo imesna inaendelea kutelezwa na NHC", alisema na kuongeza kuwa miradi hiyo pamoja na kuwa yenye ubora wa hali ya juu, gharama za kuitekeleza ni nafuu.



Mkuu wa Kitengo cha Fedha Taslimu na Miamala kwa Wateja Wakubwa na wa Kati wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Jimmy Myalize, akizungumza na baadhi ya wateja wao wa jijini Mwanza, juzi, walipokutana kwa ajili ya wakiwafahamisha kuhusu huduma mbalimbali zitolewazo na benki hiyo, pia kupata mrejesho kutoka kwao juu ya huduma hizo na jinsi wanaweza kuwahudumia vizuri zaidi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya mwezi wa huduma kwa wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Agizo la Samia lazua minong'ono

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

KUCHELEWA kutekelezwa kwa ahadi ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kuhusu uamuzi wa serikali wa kutaka kuyamega mashamba ya umma ili kutoa fursa kwa wananchi wa ukanda wa West Kilimanjaro kupata makazi ya kudumu, kumeanza kuibua minong'ono ya lini ahadi hiyo itatekelezwa.

Jana, baadhi ya wananchi wa kijiji cha Matadi, Kata ya Ndumeti, wilayani Siha wakizungumza na Nipashe, waliitaka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kufuatilia ahadi hiyo kwa kuwa wananchi wana kiu ya kujenga makazi ya kudumu.

"Tunaiomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kuweka utaratibu mzuri wa kufuatilia ahadi za viongozi wa kitaifa ambazo wanatoa wanapofika katika wilaya zetu. Changamoto kubwa ni waliopewa dhamana kukaa kimya bila kutoa mrejesho kwa wananchi," alisema Mahamoud Adinani.

Alitolea mfano ahadi ya Makamu wa Rais aliyoitoa Novemba, mwaka jana, alipotembelea wilaya hiyo kwamba haijatolewa mrejesho, hivyo kuwafanya wananchi kuanza kuhoji ukweli kuhusu kauli za viongozi wa kitaifa.

"Makamu wa Rais Samia alifanya ziara ya kikazi mkoani Kilimanjaro ambapo Novemba 18, 2018, akiwa wilayani Siha kwenye mkutano wa hadhara aliwaahidi wananchi wa eneo la Matadi kuwa atakutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Waziri wa Kilimo ili kuangalia namna ya kumega baadhi ya mashamba ya umma ili wapate makazi ya kudumu," alisema.

"Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji aliyemaliza muda wake hakutusaidia kwa kipindi chote alichokuwapo madarakani, kata yetu ina changamoto mbalimbali ikiwamo eneo la makazi ya kudumu, kituo cha afya, barabara lakini ufuatiliaji hata wa ahadi za viongozi waliohidi kutusaidia kukabiliana na changamoto hizi hakuna," alisema.

Mkazi mwingine, Kassim Mndeme, alisema viongozi wa kitaifa wamekuwa wakifika eneo hilo mara kwa mara na kutoa hadi lukuki ambazo hata hivyo huwa hazifuatiliwi na mamlaka husika.

Kwa upande wake, Ester Tarimo, alisema wanawajibika kuwakumbushia viongozi kufuatilia ahadi za wakubwa wao na kwamba ni jambo la kushangaza watu wanajitokeza kunadi sera zao haswa katika kura za maoni wakati kuna ahadi tele za viongozi wakuu hazifuatiliwi.

Diwani wa Ndumeti, Jackson Joseph, alisema tatizo la makazi kata hiyo ni la muda mrefu na kwamba ni muda muafaka kwa mamlaka husika kulitafutia ufumbuzi.


Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro (CCM), Jonathan Mabihya, alisema mchakato wa kura za maoni ndani ya mkoa huo unakwenda vizuri pamoja na kuwepo na changamoto chache zilizopelekea baadhi ya maeneo kurudiwa kwa kura za maoni.

"Unapoingia kwenye uchaguzi kuna mambo mawili kushinda na kushindwa, wako baadhi ya wagombea hawakushinda lakini hawakuridhika na matokeo hayo," alisema.

Alisema katiba ya CCM na kanuni zake, inatoa nafasi kwa mwanachama ambaye ana malalamiko yake kuyawasilisha katika ngazi husika.

"Ni kweli katika mkoa wetu tulipokea malalamiko kwa baadhi ya maeneo ambayo tayari tumeshayafanyia kazi na tayari kura za maoni zimeshafanyika katika maeneo ambayo yalionekana kuwa na changamoto," alifafanua Mabihya.

TUJIKUMBUSHE




Ukurasa 18

**Kiongozi wa IS aliyeuawa na Marekani**

Mafunzo yanavyohamasisha wanawake kuwania uongozi



Ukurasa 15



Ukurasa 14

**JAMES MAPALALA, mwanasiasa ambaye hakukata tamaa**

# siasa

JUMATANO OKTOBA 30, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 20

**Mfumo wa Iran uliowekwa Iraq, Lebanon waanza kusambaratika**

# Wenye ulemavu na uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa

- Washauri watengewe nafasi maalumu za kugombea ndani ya vyama
- Wadau washauri serikali iwatengee bajeti maalumu

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya kumalizika kwa muda wa uandikishwaji katika orodha ya wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Chama cha Wasioona (TLB) kimetoa maoni yao, huku kikipendekeza kuboresha utaratibu wa namna ya kutoa vipaumbele kwa watu wenye ulemavu katika shughuli za namna hiyo.

Rehema Hamis Darueshi ni Mratibu Idara ya Wanawake na Watoto wa Chama hicho.

Anasema bado hakuna utaratibu wa kuwatambua watu wenye ulemavu katika ngazi ya Serikali

INAENDELEA UK.16




Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo. **PICHA: MTANDAO**

**Vyama vilivyojipanga Kilimanjaro kushinda katika chaguzi zijazo** Ukurasa 19

# JAMES MAPALALA, mwanasiasa ambaye hakukata tamaa kisiasa

Na Sabato Kasika

MWANASIASA mkongwe, James Kobelo Mapalala, ambaye alifariki dunia wiki iliyopita, ni miongoni mwa wanasiasa watakaokumbukwa kwa mchango wao mkubwa kwenye siasa za nchi hii.

Kimsingi historia ya harakati za demokrasia nchini haiwezi kukamilika bila ya kutaja jina la James Mapalala, kutokana na ukweli kwamba alikuwa miongoni mwa Watanzania wa mwanzo kabisa kudai mfumo wa vyama vingi nchini.

Historia inaonyesha kwamba akiwa katika harakati za kisiasa mwaka 1968, aliandika makala katika gazeti la Kiongozi, wakati huo akiwa anaishi Tabora akielezea kutoridhishwa na mateso wanayopata wananchi wakati huo.

Alikuwa akichukizwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa vijiji wakati huo kuwatesa wananchi na akaamua kuandika kilichotokea na kujikuta akikumbana na changamoto zilizosababisha kuswekwa ndani katika vituo mbalimbali vya polisi na hatimaye kuwekwa kuzuizini

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa mwaka 1984 alimwandikia barua Mwalimu Julius Nyerere wakati wa Mkutano Mkuu wa CCM akimtaka aruhusu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi, lakini akajikuta matatani na kuwekwa kizuizini.

Mwaka 1986 alikamatwa tena na kupelekwa kizuizini mkoani Lindi, ambako alikaa hadi mwaka 1990, wakati huo akiwa amehamishiwa kisiwani Mafia mkoani Pwani.

Pamoja na matatizo hayo, hakukata tamaa kwa kuwa mawazo yake ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi yalikuwa palepale na alipotoka kizuizini, aliendeleza mawazo yake ya kuanzisha chama cha siasa.

Aliungana na wenzake na kuanzisha chama wakati ambapo hapakuwa na sheria ya vyama vingi, walienda kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, wakati huo Augustine Mrema na kumweleza nia yao hiyo.Inasemekana Mrema alikuwa mkali na akawatimua, wakaamua kuandamana wakidai haki ya kuanzisha chama cha siasa wakiwa watu 35 na walipofika maeneo ya Kariakoo, watu waliongezeka hadi kufika 1,000.

Hata hivyo, polisi waliingilia kati na kuwakamata watu 25, huku yeye (Mapalala) akikimbilia Ubalozi wa Sweden kujificha, lakini waliokamatwa waligoma kula kwa siku kadhaa na kuanza kuitisha serikali.

Kitendo cha watu hao kugoma kilisababisha aingilie kati kuwabembeleza wale chakula tena kizuri kilichotolewa Kilimanjaro Hotel na kupelekwa gerezani.

### KUANZISHA CHAMA SIASA

Wakati sakata hilo likiendelea, kulikuwa tayari kumeshajitokeza mabadiliko ya kisasa na kiuchumi ulimwenguni kufuatia mfumo wa ukomunisti kuanza kuanguka na ndipo baadaye alianzisha rasmi chama cha siasa.

Kwa ujumla, katika umri wake wa miaka 83, ambao Mungu alimjalia kuishi hapa duniani, historia inaonyesha kuwa mwanasiasa huyo alikaa kuzuizini miaka sita kwenye mikoa ya Kusini.

Hakukata tamaa, bali aliendelea na harakati zake za kisiasa bila kuchoka, kwani baada ya nchi kuridhia mfumo wa vyama vingi vya siasa, alikuwa ni miongoni mwa waanzilishi wa vyama vya siasa.

Ninaweza kusema kuwa vuguvugu la vyama vingi lilirudisha kiu ya James Mapalala ya kuwatumikia wananchi, kwani mwaka 1991 alianzisha chama cha siasa kiitwacho Chama cha Wananchi Tanzania (CCWT).

Wakati anaanzisha CCWT, kwa upande wa Zanzibar kulikuwa na Kamati ya Mabadiliko ya Kisiasa (KAMAHURU), iliyokuwa chini ya Shaban Mloo akishirikiana na Maalim Seif Sharif Hamad.

Wanasiasa wengine wa kamati hiyo walikuwa ni Ali Haji Pandu, Hamad Rashid Mohamed, Dk. Maulid Makame na Soud Yusuph Mgeni, baadaye ikawa ni chama cha siasa kiitwacho Zanzibar United Front.



Mzee James Mapalala (kulia), enzi za uhai wake akiteta jambo la Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete. **PICHA: MTANDAO**

> Mbali na Mapalala, viongozi wengine wa kwanza wa kitaifa wa CUF walikuwa, Makamu Mwenyekiti Maalim Seif Sharif Hamad wakati Katibu Mkuu akiwa ni Shabani Mloo.

### VYAMA VYAUNGANA

Mwaka 1992 baada ya kuruhusiwa kwa mfumo vya vyama vingi vya siasa, mkakati ulianza kwa kuangalia uwezekano wa kuunganisha Zanzibar United Front (ZUF) na Chama cha Wananchi (CCWT) cha Mapalala.

Historia inaonyesha Chama cha wananchi (CUF) kilianzishwa mwaka 1993 baada ya muungano wa vyama viwili; Zanzibar United Front (ZUF) kutoka Zanzibar na Chama Cha Wananchi Tanzania (CCWT) kutoka Bara.

Halmashauri kuu za vyama vyote zilikutana na kuanzisha nguvu ya pamoja mwaka huo, huku Mapalala akichaguliwa kuwa mwenyekiti wa kwanza wa CUF na alianza rasmi kazi ya kukitangaza chama Bara na visiwani.

Mbali na Mapalala, viongozi wengine wa kwanza wa kitaifa wa CUF walikuwa, Makamu Mwenyekiti Maalim Seif Sharif Hamad wakati Katibu Mkuu akiwa ni Shabani Mloo.

Hata hivyo, badala ya muungano huo kuwa na nguvu, chama hicho kiliingia katika mgogoro, kukiwa na kundi lililompinga Mapalala, ambaye alimtuhumu katibu wake kwamba alikuwa akitaka kurejesha utawala wa kisultani Zanzibar.

Mgogoro huo ulimalizika baada ya Mkutano Mkuu wa CUF kufanyika mwaka 1994 na kumtimua Mapalala, nafasi yake ilishikiliwa na Musobi Mageni aliyechaguliwa mwaka 1995.

Mageni alishikilia nafasi hiyo ya mwenyekiti wa CUF taifa hadi mwaka 1999, ambapo mwanasiasa mwingine Profesa Ibrahim Lipumba akachaguliwa kushika nafasi hiyo anayoendelea nayo hadi sasa.

Kuondolewa kwa Mapalala kulitokana na viongozi wa CUF Zanzibar kuibua hoja kwamba ni msaliti, anafanya kazi mbili, ni mwenyekiti CUF lakini pia anatumika na Chama Cha Mapinduzi (CCM) hivyo kutofaa kuwa mwenyekiti wa chama hicho.

Mgogoro wa CUF ulifika kwa msajili wa vyama wakati huo, George Liundi, ambaye pia alikubaliana na tuhuma zilizoelekezwa kwa Mapalala, hivyo ukawa mwisho wa mwanasiasa huyo ndani ya chama hicho.

### HAKUKATA TAMAA

Baada ya kutimuliwa ndani ya CUF, mwanasiasa huyo hakukata tamaa katika harakati zake za kisiasa, kwani mwaka 2001 alianzisha chama kingine kipya, Chama cha Haki na Ustawi (Chausta) akiwa ni mwanzilishi na mwenyekiti.

### BUNGE MAALUMU

Mapalala aliendelea na harakati za kisiasa, na mwaka 2014 alikuwa miongoni mwa wanasiasa walioteuliwa kuwa wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kupitia chama chake hicho cha siasa.

Moja ya kile alichokifanya katika Bunge bila kutoka kama walivyofanya wanasiasa wengine na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), ni kukataa kupigia upatu serikali mbili, katika kamati yake namba moja.

Sababu kubwa aliyoeleza kuhusu msimamo wake huo ni kwamba serikali mbili zilikuwa zinamchefua, hivyo hakutaka kushiriki katika usaliti huo wa kuunga mkono serikali mbili na alipambana humo bungeni bila kutoka ndani.

Mbali na hilo, mwanasiasa huyo akawarushia dongo wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kwamba walikuwa wakitengeneza mfumo wa kugawana posho kwa watu wa Tanzania Bara na Visiwani.

### CHAUSTA YAFUTWA

Mwishoni mwa mwaka 2016, Chausta kilikuwa miongoni mwa vyama vitatu vya siasa vilivyofutiwa usajili, vingine vikiwa ni The African Progressive Party of Tanzania (APPT-Maendeleo) na Chama cha Jahazi Asilia.

Sababu za kufutwa kwa vyama hivyo zilielezwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuwa ni kutokana na zoezi la uhakiki wa utekelezaji wa masharti ya usajili na matakwa mengine ya sheria ya vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu lililofanyika Juni hadi Julai mwaka 2016.

Baada ya uhakiki huo ilibainika kuwa vilipoteza sifa za usajili wa kudumu kwa kukiuka masharti ya sheria ya vyama vya siasa, na kila chama kilipewa nia ya msajili kufuta usajili wake, lakini vikashindwa kutoa utetezi wa kuridhisha ili visifutiwe usajili.

Kufuatia uamuzi huo, Msajili aliwataka waliokuwa wanachama wote wa vyama hivyo kutojihusisha na shughuli yoyote kwa majina ya vyama hivyo, na kwamba kufanya hivyo ingekuwa ni kuvunja sheria. Tangu kufutwa kwa Chausta katika daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa, mwanasiasa huyo hakusikika tena katika harakati za kisiasa hadi taarifa za kifo chake zilipotangazwa.

Haijulikani kama Mapalala alijiunga na chama kingine cha siasa, na huenda akikaa pembeni ili kushuhudia jinsi harakati za kisiasa zinavyoendelea nchini baada ya yeye (Mapalala) kutoa mchango mkubwa kwa miaka mingi

Hivyo kama nilieleza awali, katika siasa za nchi hii, Mapalala hawezi kuachwa pembeni, kwani ni miongoni mwa wanasiasa walipoteza muda wao ili Watanzania wawe huru kujiunga na chama chochote cha siasa wanachokitaka.

# Mafunzo yanavyohamasisha wanawake kuwania uongozi

**Na Neema Sawaka,** KISHAPU

• Ni kwenye uchaguzi Serikali za Mitaa wilayani Kishapu



Mwanasheria kutoka TGNP, Theresia Sawaya(aliyesimama), akizungumza katika mafunzo ya uongozi kwa wanawake watia nia ya kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kutoka vitongoji na vijiji vya baadhi ya kata za wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga. **PICHA: MTANDAO**

Distributed via ippmedia

UCHAGUZI wa Serikali za Mitaa unaofanyika Novemba 24 mwaka huu, umefanya baadhi ya mashirika likiwemo la Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kuratibu mafunzo maalumu.

Ni mafunzo ya kuwajengea wanawake uwezo, ujasiri na mbinu ya kuingia na kupambana katika kinyang'anyiro cha uchaguzi huo kwa lengo la kushinda.

Mwanasheria Theresia Sawaya kutoka TGNP, aliyekuwa mwezeshaji kwa wanawake wanaotarajia kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa serikali za mitaa kugombea nafasi mbalimbali ndani ya vyama vyao wilayani Kishapu, ananena.

Sawaya anasema wameamua kuwajengea uwezo na mbinu za kuwafanya waondoe hofu, hatua itakayovunja suala la mfumo dume uliopo ndani ya jamii.

Akiwa ni mwezeshaji wa wanawake zaidi ya 60 waliotia nia ya kuwania uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, Sawaya anawataka wanawake waondoe usiri.

Kwamba wasifanye siri kwa waume zao au ndani ya familia zao ambako ndiko kuna vikwazo vinavyowafanya wagombea wanawake, hasa walioolewa kukata tamaa ya kugombea nafasi za uongozi.

"Ninawakumbusha watia nia ya kuwania uongozi kuwa wawazi, kushirikisha wananchi wanaowazunguka, kwamba hata kama hawakupendi, fanya ushawishi wafahamu malengo yako na hasa utafanya nini ukipata nafasi hiyo unayoitaka," anasema.

Anabainisha kwamba kuna baadhi ya wanawake ambao wamekuwa wakitia nia ya kugombea kwenye chaguzi mbalimbali, lakini hushindwa kujieleza.

"Ni bora basi kujiandaa mapema, kusoma mazingira ya kujieleza vizuri, kuandaa mpango kazi na raslimali fedha hata kwa kuomba, ila isiwe rushwa ambayo ina madhara baadaye," anasema na kuongeza:

"Shirikisha jamii, familia kama mume wako, pia shirikisheni viongozi wa dini bila kusahau vyombo vya habari ili taarifa zako zifike mbali."

Naye Evahawa Juma, mwanasheria vilevile kutoka TGNP, anasema lengo mahsusi ya mafunzo hayo lisiwe kugombea tu nafasi za uongozi kwenye vyama vya siasa, bali hata kwenye vikundi vya kijamii.

"Wanawake wengine wamekuwa wakishindwa kuongoza hata vikoba, na wenzao wanapojitokeza kuongoza husemwa kwamba hawawezi badala ya kuwatia moyo," anasema na kuongeza:

"Tukishikamana tunaweza, idadi yetu ni kubwa kuliko wanaume...neno wanawake hatupendani liondoke, tushikamane hata kwenye uchaguzi unaokuja" anasema.

> Ni bora basi kujiandaa mapema, kusoma mazingira ya kujieleza vizuri, kuandaa mpango kazi na rasilimali fedha hata kwa kuomba, ila isiwe rushwa ambayo ina madhara baadaye.

### WAWANIA UONGOZI

Angelina Mahona (30) ambaye ameongoza katika kura za maoni kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi ( CCM), anasema anatarajia kuingia katika kampeni ili aweze kuibuka mshindi.

Anawania nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji cha Nhobola, Kijiji cha Bulimba, Kata ya Ukenyenge, wilayani Kishapu.

Angelina anasema haikuwa rahisi kuwashinda wapinzani wake wanne aliokuwa akishindana nao kwenye kura za maoni, baada ya kupata kura 14, akifuatiwa na mwanaume aliyepata kura 12.

Angelina anabainisha ni ujasiri uliomfanya afikie hatua hiyo.

Anasema awali alikuwa mjumbe wa serikali ya kijiji na alishawishika kuwania nafasi hiyo ya uenyekiti wa kitongoji baada ya kuona anafaa kuwatumikia wananchi na kuwa nao bega kwa bega kutatua changamoto zinazowakabili.

"Kihistoria nimekutana na changamoto nyingi za kimaisha ndani ya familia, umaskini, kukosa msaada katika jamii na mbaya zaidi nilipomaliza darasa la saba na kufaulu, wazazi walidai hawawezi kusomesha mtoto wa kike," anasema.

Anabainisha kwamba akiwa na umri wa miaka 17 tayari alikuwa kapata mtoto na aliolewa kwa sababu hakuwa na namna ya kufanya.

"Pamoja na hayo nilijielekeza pia kanisani, ambapo nilikuwa nikimshirikisha mchungaji wa kanisa aliyenitia moyo kuwa jasiri," anasema na kuongeza:

"Nilijiunga na uimbaji wa kwaya ya Kanisa la KKKT, lililo Kijiji cha Negezi, Kata ya Ukenyenge, wilayani Kishapu."

Angelina anasema baada ya kuonekana kanisani ana juhudi ya kuweza kuwasimamia wengine, uongozi wa kanisa hilo ulimkabidhi mtaa wa eneo la kanisa na waimbaji wenzake.

"Na mtaa ulionekana kwenda vizuri, kwaya haikuyumba na mpaka nikatunukiwa zawadi ya baiskeli," anasema.

### ANNE MAKINDA

Angelina anasema angependa kufikia mafanikio ya aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Anne Makinda, aliyeliongoza Bunge vyema na kwa mafanikio.

Anasema ameisoma historia ya Spika huyo mstaafu kwenye majarida na vitabu mbalimbali vilivyoanisha changamoto nyingi alizokumbana nazo katika familia yake, lakini alisimama imara na kwa ujasiri akapambana na changamoto hadi kufikia nafasi ya juu ya mojawapo ya mhimili ya dola, yaani Bunge.

"Nami naamini siku moja nitakuwa kama mama Makinda," anasema.

Akizungumzia mtazamo wa mumewe kuhusiana na hatua yake ya kugombea uongozi, Angelina anasema hajapata vikwazo vyovyote kutoka kwa mume wake sababu nafasi anayoiwania ya uenyekiti wa kitongoji ilikuwa inashikiliwa na mumewe huyo.

### ESTHER LUGONDEKA

Huyu ni mwanamke mwingine aliyepita kwenye kura za maoni kwa tiketi ya CCM, akiwania nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji cha Shishinulu, Kijiji cha Negezi, Kata ya Ukenyenge wilayani Kishapu.

Anasema amekumbana na kikwazo kutoka kwenye jamii kinachojaribu kumuonyesha kwamba mwanamke hawezi kutumikia mabwana wawili, yaani familia na uongozi pindi atakapohitajika kwenye majukumu.

### DIWANI

Diwani wa viti maalumu Suzana Makoye ambaye alishawahi kuwa Katibu Tarafa ya Mondo, wilayani Kishapu, anatoa ushuhuda wa alivyokuwa akipewa vikwazo na mume wake vya kumkatisha tamaa.

"Mume wangu alikuwa akinipa nadharia kwamba haiwezekani mimi kuwa diwani kwa sababu nimetoka kwenye wadhifa wa juu na kuja kugombea nafasi ya chini, kwamba ni kujidhalilisha," anasema na kuongeza"

"Sikuvizingatia vikwazo hivyo, kwani nilichojua familia yangu inakwenda vizuri na nitaweza kuitumikia jamii endapo nitapewa nafasi na ndicho kilichotokea... sasa mume wangu ananiunga mkono na ananipa ushirikiano katika kuitumikia jamii."

Hali iko hivyo vilevile kwa Sara Masinga ambaye naye ni Diwani wa viti maalum kutoka wilaya ya Kishapu.

Anasema alishirikisha familia yake ukiwemo uongozi wa kanisa na kufanikiwa kupata nafasi hiyo.

### ELIZABETH LWENGE

Elizabeth naye ni Diwani wa viti maalum ambaye anabainisha kupata vikwazo kutoka kwenye jamii mwaka 2010, alipokuwa akigombea nafasi ya uenyekiti serikali za mitaa.

"Nilinyoshewa kidole kuwa sina sera ninayoenda kuisimamia zaidi ya kwenda kujiuza...hata mume wangu alianza kuniwekea vikwazo akinitaka niwaachie wanaume kwani ndio wanaoweza kukabiliana hata na migogoro inayotokea nyakati za usiku," anasema na kuongeza:

"Jamii iliniona kama nisiyefaa kuongoza, ikisema mama huyu hataki kuishi na mume wake anataka kuvunja mji wake."

Elizabeth anasema si kwenye jamii tu bali na ndani ya familia, kwenye vyama, kote huko kuna changamoto vilevile pale mwanamke anapokwenda kuchukua fomu ya uongozi.

# Wenye ulemavu na uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa


Distributed via ippmedia

Semina kama hizi muhimu kwa walemavu wa macho katika kuwajengea ujasiri na fursa za kushiriki katika shughuli mbalimbali zikiwamo za uchaguzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

za Mitaa na kuwapa kipaumbele katika shughuli muhimu zikiwamo za uchaguzi.

Rehema anasema katika kipindi hicho cha kujiandikisha, baadhi ya watu wenye ulemavu walipata changamoto ya kutokana na mazingira waliyonayo ya kutoona.

Anasema miongoni mwa sababu zilizochangia baadhi ya watu wenye ulemavu kushindwa kujiandikisha kwa ajili ya maandalizi ya kupiga kura kuchagua viongozi wa ngazi hiyo Novemba 24 mwaka huu, ni pamoja na kukosa wasindikizaji, pia elimu ya uraia kwa kundi hilo.

"Katika kipindi cha uandikishaji hali haikuwa nzuri sana kwa watu wenye ulemavu hususani wasioona...kwa mfano katika jiji la Dar es Salaam katika kipindi cha uandikishaji, kulikuwa na mvua nyingi, hivyo mtu kama mimi ambaye sioni, inakuwa ngumu kumudu hali hiyo," anasema na kuongeza:

"Pili, sisi kutembea kwetu huwa lazima tuwe na mtu wa kutusindikiza au kutuongoza... kwa hiyo wakati mwingine mtu unayemtegemea kwamba akusindikize halafu naye akawa ametingwa na shughuli zake nyingine, tayari unakuwa umekwama."

sababu ya tatu anayoitaja Rehema ni kwamba, wengi wa watu wenye ulemavu bado hawana elimu ya kutosha ya uraia juu ya ushiriki wao katika mambo haya muhimu kitaifa.

"Mara nyingi huwa wanajiona hawahusiki au wanajitoa katika mambo muhimu, na hii yote ni kwa sababu ya kukosekana kwa elimu ya uraia... kwa mfano katika masuala ya uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ina kazi ya kufanya hapa, itoe elimu kwa kundi hili," anasema.

> Ifike mahali kundi hili nalo lipewe kipaumbele... tatizo watu wanawachukulia wenye ulemavu kama ambao hawana uwezo, hili siyo sawa.

Rehema anataja sababu nyingine inayochangia kundi hili la watu wenye ulemavu wasijitokeze kwa wingi ni la wao kujinyanyapaa.

"Na hali hiyo ya watu wenye ulemavu kujiona hawafai, chimbuko lake ni jamii kwa sababu mpaka sasa nchi yetu bado haina imani na mtu mwenye ulemavu, na ndiyo maana anapozaliwa tu anaanza kunyanyapaliwa na wengine huwaficha ndani kabisa," anasema na kuongeza:

"Kwa hiyo na wenyewe walifika mahali wakajiona hawafai, wakaanza kujinyanyapaa hata kama hawajanyanyapaliwa...ndiyo maana ni muhimu kwa minajili ya kuondoa hii hali kwa kundi hili ni lazima familia, jamii na hata serikali ifanye kazi ya ziada kuondoa imani hiyo, kwa kuwaonyesha upendo na kuwapatia upendeleo wa juu kivitendo na hasa katika vipindi kama hivi vya uchaguzi."

Rehema ambaye pia ni mwalimu wa shule ya msingi Tuangoma wilayani Temeke, anasema yeye alipata bahati ya kujiandikisha baada ya shule kuwawekea utaratibu mzuri wenye ulemavu kwa kuwafuata katika maeneo yao ya kazi.

"Kwa kweli nipongeze utaratibu uliofanywa na uongozi wa shule yetu, wa kuzungumza na serikali za mitaa tunakotoka ili wafike shuleni kuja kutuandikisha,"anasema.



Wananchi wakiwa katika foleni ya kuchagua viongozi wao.

Anashauri kwamba ni vema serikali za mitaa husika zikaweka utaratibu wa kuwatambua watu wenye ulemavu katika mitaa yao.

Anasema, hiyo ni la msingi ili kunapotokea shughuli mbalimbali muhimu zinazohitaji ushiriki wao hususani za uchaguzi na nyinginezo, kundi hilo liwe limewekewa utaratibu wake maalum wa kushiriki badala ya kukaa kimya bila kufahamu kama wanashiriki au la.

"Utaratibu huu utawezesha kupata sauti ya kundi hili, hata ikiwezekana wakodishiwe usafiri wa kuwafikisha mahali ambapo ushiriki wao unahitajika," anasema na kuongeza"

"Ifike mahali kundi hili nalo lipewe kipaumbele... tatizo watu wanawachukulia wenye ulemavu kama ambao hawana uwezo, hili siyo sawa."

## MRATIBU

Mratibu Idara ya Maendeleo ya Vijana na Chipukizi wa TLB, Kiongo Itambu, anasema yeye kama kiongozi kwenye chama hicho, anaona bado kunahitajika nguvu ya ziada kupambana na fikra na imani za Watanzania juu ya watu wenye ulemavu.

Itambu anabainisha kuwa watu bado wanaamini kwamba mtu mwenye ulemavu hawezi kuwa na uwezo wa kufanya lolote na si lazima kumshirikisha.

"Imani hii ipo kuanzia hata katika familia zetu, pamoja na kwamba siku hizi elimu inatolewa watu waondokane na imani hizo, lakini bado hali ni ngumu kwetu... unakuta hata katika familia tunakotoka kuna jambo muhimu la kujadili, lakini hatushirikishwi... kadhalika kwenye nyanja mbalimbali za maamuzi serikalini, japo sasa hivi tunaona angalau tumeanza kupewa nafasi,"anasema.

Anaongeza: " Kwa mfano mimi ni mwanachama wa chama cha siasa, nimekuwa nikishuhudia katika nafasi mbalimbali tunapotaka kugombea ndani ya chama hatupewi kipaumbele. Si kwamba wanatukataza kugombea isipokuwa wanatuacha tugombee, lakini inapofika kwenye kura za maoni hatupitishwi."

Itambu anafafanua kwamba huwa kuna kampeni za chinichini zinazofanyika ili waachwe wagombee lakini wasipigiwe kura za maoni za kuwapitisha, sababu kubwa ikidaiwa kwamba watapoteza nafasi, iwe ni katika mitaa, udiwani au ubunge.

"Niliwahi kugombea Udiwani lakini nilipigwa vita kwenye kura za maoni, nikashindwa na wasio na ulemavu, wakihofia kupoteza nafasi hivyo hivyo, wengine wakisema sasa huyu hata akichaguliwa ataongozaje...kwa hiyo bado tuna kazi kubwa ya kufanya katika hili," anasema.

## WITO

Itambu anasema ni vema ikafika wakati, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ikaweka sheria ya kuvilazimisha vyama kuweka utaratibu ambao utaondoa vikwazo vyote kwa kundi la watu wenye ulemavu kuwania nafasi ndani ya vyama vya siasa.

"Sheria hiyo kwa vyama vya siasa, iweke nafasi maalum ambazo zitakuwa za kundi hilo zitakazoshindaniwa na wenyewe, kama ziko tano, wajitokeze wenye ulemavu wapambane na kupigiwa kura, lakini si kuwaacha wapambane na wasio na ulemavu," anasema na kuongeza:

"Hapa kutakuwa hakuna ile tabia ya chama kusema oohh tutapoteza mtaa, kata au Jimbo, kwa sababu nafasi zitakuwa zimewekwa kabisa, na hapa ndiyo itakuwa mwanzo wa kundi hili kuonekana na kuonyesha uwezo wao na naamini kwamba haya yanawezekana."

Itambu anasema hilo si jambo baya kwani ni sawa na anapojiunga na uanachama, kwani huwa wanapokelewa na kulipa ada zote, hivyo haoni sababu inapofika kwenye suala la kugombea, kunakuwa na hofu ya chama kupoteza nafasi.

"Hii siyo haki kabisa,"anasema.

## MENEJA

Meneja Utafutaji Rasilimali wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Naemy Silayo, anasema kugombea nafasi zozote katika ngazi ya siasa ni haki ya kila mtu, hivyo kundi hilo linastahili haki hiyo kama yalivyo makundi mengine.

Silayo anasema ni vema serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikaweka mfumo ambao utavilazimisha vyama kuwa na nafasi maalum za kundi la watu wenye ulemavu.

"Na mfumo huo uweke masharti kwamba chama chochote kitakachoshindwa kutenga nafasi kwa wenye ulemevu, kifutiwe usajili... lazima ifike wakati tuone umuhimu wa kundi hili kwani si jambo jema kuacha kumwamini mtu wakati hujamjaribu... unaweza ukamnyima mtu nafasi kwa kusema humwamini na ukampatia mwingine unayesema unamwamini, ndiyo akawa mbaya kuliko yule uliyesema humwamini," anasema.

Anashauri kwamba kutokana na changamoto mbalimbali ambazo kundi hili hukutana nazo, ni vema vilevile kukawa na utaratibu maalum kwa serikali kuwatengea bajeti ambayo itakuwa inashughulikia gharama katika vipindi vya shughuli zinazohitaji ushiriki wao.

## TAMISEMI

Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mwita Waitara, anasema katika hili kwamba tayari Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeshalitolea ufafanuzi.

> ...Tatizo watu wanawachukulia wenye ulemavu kama ambao hawana uwezo, hili siyo sawa.

"Haya ni miongoni mwa mambo ambayo yametolewa mwongozo na Katibu Mkuu wa CCM Dk. Bashiru Ally, lengo likiwa ni kuhakikisha anachaguliwa kiongozi bora bila kujali hali aliyonayo ili mradi awe amethibitika kuwa ana sifa za kuwa kiongozi bora," anasema.

## NEC

Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Omary Mafuli, anasema Tume hiyo imekuwa ikikutana na makundi mbalimbali kutoa elimu ya uraia, lengo likiwa ni kuhakikisha kila kundi linashiriki katika uchaguzi.

# DRC yatakiwa kulinda kivitendo watu wa asili



Rais Felix Tshisekedi wa DRC. **PICHA: MTANDAO**

MTAALAM maalum wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu haki za watu wa jamii za asili, Victoria Tauli-Corpuz, amehitimisha ziara yake ya siku 11 nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kusisitiza umuhimu wa serikali hiyo kutekeleza kwa vitendo sheria ya kuheshimu haki za jamii hiyo.

Katika ripoti yake iliyotolewa na Ofisi ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (OHCHR), mwishoni mwa ziara yake, mtaalam huyo amesema anashukuru na kutambua hatua za serikali ya DRC ya kupitisha sheria namba 5 ya mwaka 2011, ili kuendeleza haki hizo.

Haki hizo zikiwamo za elimu, kijamii na hata umiliki wa ardhi lakini bado kuna changamoto kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa sheria hiyo iliyopitishwa mwaka 2015.

Amesema ingawa maofisa wa serikali wamekuwa mara kwa mara wakimhakikishia kuwa kuna utashi wa kisiasa wa kutekeleza sheria hiyo ambayo hata mwaka 2017, kulitolewa msururu wa maagizo ya kutekeleza, bado kuna vikwazo. Tauli-Corpuz anatoa mfano wa ziara yake huko Kabo ambako kuna shule yenye wanafunzi 140 wa jamii ya asili, lakini ina walimu watatu ambao wote si wa jamii ya asili.

Mtaalam huyo amesema anaamini kuwa uwepo wa utashi wa kisiasa kutekeleza sheria hiyo ya kuendeleza haki za jamii ya asili, uende sambamba na kutenga bajeti ili kuweza kupata rasilimali zinazohitajika kuwawezesha wapate haki zao.

"Nasisitiza tena mapendekezo yaliyotolewa na mtangulizi wangu kuwa mifumo ya kimsingi iliyowekwa ya kubagua watu wa jamii ya asili, inahitaji ushiriki sahihi wa kijamii ili iweze kutambulika na hatua zichukuliwe kujenga heshima baina ya watu wa jamii zote nchini DRC," anasema.

Anakumbusha kuwa kukabili changamoto hizo za elimu na nyinginezo kwenye afya na hata jamii hizo kushiriki kwenye miradi inayoweza kuathiri maeneo yao, kunawezekana tu pale ambapo kuna juhudi za pamoja zikileta pamoja serikali, mashirika ya kiraia na wadau wengine wa maendeleo na watu wenyewe wa asili.

Anakumbusha kuwa wanaweza kuchangia maarifa yao ya asili katika usimamizi wa rasilimali asili, mabadiliko ya tabianchi na tiba za asili.

Wakati wa ziara hiyo inayotokana na mwaliko wa serikali, mtaalam huyo alikutana na viongozi wa serikali, mashirika ya kiraia, UN na watu wa jamii ya asili. **HABARI UN**

TUJIKUMBUSHE

# ABU BAKR AL-BAGHDADI

## • Kiongozi wa IS ambaye ameuawa na Marekani

ABU Bakr al-Baghdadi, Kiongozi wa kundi la Kijihad la Islamic State (IS) na mtu ambaye alikuwa akisakwa sana duniani, alijiua kufuatia uvamizi wa Marekani uliotekelezwa na kikosi maalum cha wanajeshi Kaskazini Magharibi mwa Syria, kulingana na Rais Donald Trump.

Kiongozi huyo aliyejiita 'Kalifa Ibrahim' alikuwa amewekewa dola milioni 25 kwa mtu yeyote ambaye angefichua maficho yake na alikuwa akisakwa na Marekani na washirika wake, tangu kuanzishwa kwa kundi la IS miaka mitano iliyopita.

IS lilidhibiti kilomita 88,000 mraba za eneo kutoa Magharibi mwa Syria hadi Mashiriki mwa Iraq, na likaweka utawala wake wa kikatili kwa zaidi ya watu milioni 8, huku likijipatia mabilioni ya dola kutoka kwa mapato ya mafuta, wizi na utekaji nyara.

Lakini licha ya kuangamizwa kwa utawala wao na kiongozi wake, IS inasalia kuwa kundi kali la kivita na kikosi chenye nidhamu ya hali ya juu, ambapo kuangamizwa kwake hakuna uhakika.


Distributed via ippmedia

### 'ALIYEAMINI'

Jina lake Baghdadi, ni Ibrahim Awwad Ibrahim al-Badri na alizaliwa mwaka 1971, katika mji wa kati wa Iraq kwa jina Samarra.

Familia yake ni ya Waarabu wa madhehebu ya Sunni, inayodaiwa kutoka katika kabila la mtume Muhammad la Quraysh, kitu kinachoaminika kuwa sifa ya kuwa Kalifa.

Akiwa kijana, alipewa jina la utani 'Muumin' na nduguze kwa kuwa alihudumia muda wake mwingi akiwa ndani ya msikiti akisoma Quran na kwamba mara kwa mara aliwashutumu walioshindwa kufuata sheria ya Kiislamu au sharia.

Baada ya kumaliza shule mapema miaka ya 1990, alielekea katika mji mkuu wa Baghdad. Alijipatia shahada na shahada ya uzamivu katika mafunzo ya Kiislamu kabla ya kusomea stashahada katika chuo kikuu cha Kiislamu cha Baghdad. Kulingana na wasifu wake uliochapishwa na wafuasi wake.

Akiwa mwanafunzi aliishi karibu na msikiti wa Kisunni katika mji wa Kaskazini Magharibi mwa Baghdad, wilaya ya Tobchi.

Anasemekana kuwa mtu mtulivu aliyewekuwa msiri wa mambo yake isipokuwa wakati alipokuwa akijifunza kusoma Quran na kuichezea soka klabu ya msikiti huo.

Baghdadi anaaminika kukumbatia Jihad na salafi wakati huo.

### 'CHUO KIKUU CHA KIJIHADI'

Kufuatia mashambulizi ya Marekani yaliyompindua Rais Saddam Hussein 2003, Baghdadi aliripotiwa kuanzisha kundi la wapiganaji wa Kiislamu kwa jina Jamaat Jaysh Al al- Sunnah wa-al-Jamaah ambalo lilishambulia vikosi vya Marekani na washirika wao.

Ndani ya kundi hilo, alikuwa kiongozi wa kamati ya sharia. Mapema 2004, Baghdadi alikamatwa na wanajeshi wa Marekani katika mji wa Faluja, Magharibi mwa Baghdad, na kupelekwa katika kambi moja ya Bucca Kusini.

> Mapema mwaka 2006, Al Qaeda iliunda baraza la Jihad kwa jina Mujahideen Shura, ambalo kundi hilo la Baghdad liliahidi kutii na kujiunga nalo.

Kambi ya Bucca ilikuwa kile ilichoelezewa kuwa chuo cha viongozi wa siku zijazo, huku wafungwa wakipewa itikadi kali na kupata mawasiliano muhimu.

Baghdadi aliripotiwa kuongoza ibada, alitoa hotuba na kufunza madarasa ya kidini akiwa kizuizini na mara nyingine alitakiwa kuingilia kati ili kutatua mizozo na utawala wa Marekani katika kambi hiyo.

Hakuonekana kama mwenye tishio kubwa kwa Marekani na alitolewa baada ya miezi 10.

"Alikuwa mhalifu wa barabarani tulipomkamata 2004, Ni vigumu kufikiria kwamba atakuwa kiongozi wa IS," Ofisa mmoja wa Pentagon aliliambia gazeti la The New York Times 2014.

### KUUNDA AL-QAEDA NCHINI IRAQ

Baada ya kuondoka kambi ya Bucca, Baghdad anaaminika kuwasiliana na uongozi mpya wa al-Qaeda nchini Iraq.

Chini ya uongozi wa Abu Musab al - Zarqawi, Al - Qaeda lilibadilika na kuwa kundi kubwa katika uvamizi huo wa Iraq na kupata sifa kwa ukatili wake, ikiwamo kuchinja watu vichwa.

Mapema mwaka 2006, Al Qaeda iliunda baraza la Jihad kwa jina Mujahideen Shura, ambalo kundi hilo la Baghdad liliahidi kutii na kujiunga nalo.

Baadaye mwaka huo, kufuatia kifo cha Zarqawi aliyefariki kutokana mashambulizi ya angani ya wanajeshi wa Marekani, shirika hilo lilibadili jina lake hadi kundi la Islamic State nchini Iraq.

Baghdadi alisimamia kamati ya ISI na kujiunga na baraza hilo la Shura.

Wakati kiongozi wa ISI Abu Umar al- Baghdadi alipofariki kutokana na mashambulizi ya Marekani ya 2010 pamoja na naibu wake Abu Ayyub al- Masri, Abu bakr al- Baghdadi, alitajwa kuwa mrithi wake.

Alirithi shirika ambalo makamanda wa Marekani waliamini linakaribia kushindwa.

Lakini kupitia usaidizi wa wanajeshi kadhaa wa Saddam na maofisa wa Kijasusi, miongoni mwao wafungwa wenza wa kambi ya Bucca alianza kuijenga upya ISI.

### 'KALIPHA IBRAHIM'

Mapema 2013, lilikuwa likitekeleza mashambulio kadhaa kwa mwezi nchini Iraq.

Pia lilishiriki katika pingamizi dhidi ya utawala wa Rais Bashir Assad, akituma wanajeshi wa Syria kurudi Iraq baada ya kuunda kundi la al- Nusra Front kama mshirika wa al- Qaeda nchini humo.

Wakiwa hapo waliweza kupata silaha kwa urahisi.

Mwezi Aprili, Baghdadi alitangaza kuunganishwa kwa vikosi vyake nchini Iraq na Syria na uundaji wa kundi la Islamic State (IS) nchini Iraq na lile la ISIL.

Viongozi wa al - Nusra na al-Qaeda walikataa hatua hiyo, lakini wapiganaji walio watiifu kwa Baghdad walijiondoa katika al-Nusra na kulisaidia ISIS kusalia Syria.

Mwisho wa mwaka 2013, IS ilirudi Iraq na kusababisha hali ya sintofahamu kati ya serikali ya madhehebu ya Kishia na walio wachache wa madhehebu ya Sunni walio Waarabu.

Wakisaidiwa na makabila yao na waliokuwa wandani wa Rais Saddam Hussein, ISIS iliiteka Faluja.

Mwezi Juni 2014, wanajeshi kadhaa wa ISIS waliteka mji wa Mosul, wakilifukuza Jeshi la Iraq na baadaye kuelekea Kusini mwa Baghdad, wakiwaua wapinzani wao na kutishia kuyaangamiza makabila mengi ya walio wachache.

Mwisho wa mwezi, baada ya kuteka makumi ya maeneo ya miji ya Iraq, ISIL ilitangaza uongozi wa Kiislamu, taifa linaloongozwa kwa mujibu wa sharia za Kiislamu na kulitaja kuwa taifa la Kiislamu Islamic State.

Ulimtangaza Baghdadi kama Kalipha Ibrahim na kutaka utiifu kutoka kwa Waislamu wote duniani.

Siku tano baadaye, kanda ya video ilitolewa ikimuonyesha Baghdadi akitoa hutuba katika msikiti mkuu wa Mosul wa al- Nuri, ikiwa mara yake ya kwanza kuonekana katika kamera.

Wataalam walisema kwamba hotuba za Baghdadi zilifanana na hotuba zilizotolewa na makalifa wa karne ya kwanza wa Kiislamu.

Aliwaomba Waislamu duniani kuhamia katika eneo la Islamic State ili kusaidia Waislamu kupigana dhidi ya wasioamini. Makumi ya maelfu ya wageni walielekea katika eneo hilo ili kuitikia wito huo.

Mwezi mmoja baadaye, wapiganaji wa IS waliingia katika maeneo yanayodhibitiwa na Wakurdi walio wachache nchini Iraq na kuwaua mbali na kuwateka maelfu ya watu wa kabila hilo wanaotoka katika dini ya Yazidi.

Ukatili huo dhidi ya Yazidi, ambao wachunguzi wa Umoja wa Mataifa (UN) walisema unashirikisha uhalifu wa kimbari, ulisababisha kuundwa kwa muungano unaoongozwa na Marekani ambao ulianza kampeni ya angani dhidi ya wapiganaji wa kijihadi nchini Iraq. Muungano huo ulianza mashambulizi ya angani nchini Syria mwezi Septemba, baada ya IS kuwachinja mateka kadhaa wa Magharibi.

IS ilijibu mashambulizi ya moja kwa moja dhidi ya muungano huo unaoongozwa na Marekani, wakiutaja kama vita dhidi ya adui wa Waislamu vilivyotabiriwa na hadithi za mitume.

Katika maeneo yaliyopo chini ya udhibiti wake, IS iliweka sheria ya Kiislamu iliyokuwa ikiwanyanyasa wakazi.

Wanawake waliotuhumiwa kushiriki ngono nje ya ndoa walipigwa mawe hadi kufa, mikono ya wezi ilikatwa huku wale waliotuhumiwa kupinga uongozi wa IS walikatwa vichwa.

Rubani mmoja wa Jordan ambaye ndege yake ilianguka karibu na Raqqa, Luteni Moaz al-Kasasbeh alichomwa moto hadi kufa.

**BBC**

**ITAENDELEA**

# Vyama vilivyojipanga Kilimanjaro kushinda katika chaguzi zijazo

**Na Mary Mosha,** KILIMANJARO

NOVEMBER 24, mwaka huu, utafanyika uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini.

Kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro, kunatarajiwa kuchaguliwa wenyeviti wa Mitaa 60, vijiji 519 na vitongoji 2,260, huku kukiwa na vituo vya uandikishaji 2,362.

Miongoni mwa vyama vya siasa vinavyotarajiwa kushiriki katika uchaguzi huo mkoani Kilimanjaro ni pamoja na NCCR Mageuzi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Vyama vyote vya siasa vimeendelea kujigamba kuwa, kila kimoja kitashinda kwa kishindo kwenye uchaguzi huo, na hivyo kujiweka katika nafasi nzuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu, unaotarajiwa kufanyika Oktoba 25, mwakani.

Pamoja na majigambo hayo, vyama shiriki vya upinzani vinaonyesha wasiwasi kwa wagombea wao kutotangazwa endapo watashinda.

Vinatoa msimamo huo vikidai kuwa inatokana na matamko ambayo yamekuwa yakitolewa na baadhi ya viongozi wa Serikali na CCM, kuwa chama hicho kitashinda kwa namna yoyote.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira. **PICHA: MTANDAO**

### NCCR

Katibu Mwenezi wa NCCR Mageuzi Taifa, Hemedi Msabaha, anasema wamejipanga kushiriki kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mujibu wa katiba na kanuni.

Msabaha anasema, hiyo ni licha ya kuwa kinaamini kinakabiliwa na changamoto kubwa ya utaratibu na usimamizi kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa uandikishaji.

Anasema chama chao kimejipanga kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo, na wanatarajia kushinda licha ya kuwa na changamoto za kimfumo, hasa kutokana na baadhi ya viongozi ambao hawamo kwa mujibu wa sheria.

Anabainisha kwamba, chama chao kinaona viongozi kama hao wanaoingilia uchaguzi huo kwa kutoa matamko mbalimbali pamoja na kuwaaminisha wananchi kwamba wagombea wa CCM, watashinda kwa namna yoyote ile.

"Mwaka 2014, kulikuwa na Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), lakini katika jimbo la Vunjo tulifanikiwa kushinda vijiji 27 kati 78 na kwa sasa tunatarajia kushinda vijiji vyote na mitaa kwa asilimia 86 kwa Mkoa wa Kilimanjaro," anasema na kuongeza:

"Kwani majimbo na wilaya zote tumesimamisha wagombea na kwa takwimu tutaziweka wazi... tunaingia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, tukiamini tuna changamoto nyingi hasa za vitisho."

Msabaha anadai mfumo wa kiuchaguzi umeingiliwa na baadhi ya viongozi ambao hawastahili kuingia kwenye uchaguzi na matamko ya baadhi ya viongozi wa chama tawala, yanaleta hofu ili wakate tamaa.

"Hata hivyo, hatutakata tamaa... kitendo hichi hakitafanyika kwa mara ya kwanza, kwani katika jimbo la Vunjo kwenye uchaguzi wa mwaka 2014, katika kijiji cha Duhuni, Kirua Vunjo Magharibi, alitangazwa mgombea ambaye hakushinda kihalali," anasema na kuongeza:

> Tunatarajia kuendeleza historia kutokana na jitihada anazofanya mwenyekiti wa chama Taifa, Rais John Magufuli.

"Hali hiyo ilisababisha uvunjifu wa amani, miongoni mwa wananchi, kitendo ambacho si kizuri na kinakwamisha maendeleo."

### CCM

Kwa upande wake, Jonathani Mabia, Katibu wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, anasema wamejipanga vyema kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, Novemba 24.

Anasema chama hicho tayari kimemaliza mchakato wa kupata wagombea wa chama watakaoshiriki katika kinyang'anyiro hicho, ngazi ya serikali za mitaa.

Anabainisha kutokana na utendaji uliotukuka wa serikali ya awamu ya tano, wanatarajia kushinda kwa asilimia 100.

"Sisi kama watendaji, tumehakikisha tumechagua viongozi wanaokubalika na wananchi katika kujituma na kuwaletea maendeleo... hatuna mashaka ya kushinda katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sababu kupitia Ilani ya CCM na utendaji wa serikali, umewaridhisha wananchi," anasema.

Mabia anabainisha kwamba kwenye chaguzi za mwaka 2014, ngazi ya serikali za mitaa, chama hicho kiliongoza kwa kupata idadi kubwa ya vijiji, vitongoji na mitaa.

"Tunatarajia kuendeleza historia hiyo kutokana na jitihada anazofanya mwenyekiti wa chama Taifa, Rais John Magufuli,"anasema.

Anabainisha kwamba wao wanashiriki kwenye uchaguzi huu kwa mujibu wa sheria na kuionyesha dunia kuwa wanatekeleza demokrasia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

### TUHUMA ZA VYAMA VYA UPINZANI

Akizungumzia tuhuma za vyama vya upinzani juu ya kutangazwa kwa wagombea hata kama hawatashinda, Mabia anasema hilo halitegemewi.

"Vyama vyote vina uhuru wa kuweka mawakala wa kulinda hesabu na kusimamia kura za wagombea wao...lakini pia suala la kutangaza si la chama bali ni la kisheria," anasema na kuongeza:

"Chama kimefanya mambo makubwa kwa wananchi, hivyo hatutegemei kushindwa na badala yake tunatarajia ushindi wa asilimia 100."

Mabia anatoa rai kwa vyama vya upinzani kutoogopa kuingia uwanjani, kwamba la muhimu kwa wote ni kufuata sheria na taratibu za uchaguzi, ili hatimaye apatikane mshindi atakayeweza kuwatumikia vyema wananchi.

"Tunasikia baadhi ya viongozi wanalalamika kuhusu muda uliowekwa wa kampeni, lakini CCM tunasema muda uliowekwa wa siku saba unatosha kwa sababu viongozi wanaochaguliwa wapo katika maeneo ya wananchi ambao wanajua nini wamewatendea," anasema.

### CHADEMA

Kwa upande wake, Chadema kinabainisha kwamba kutokana na jitihada walizofanya wanatarajia kupata ushindi kwa asilimia 80, katika mkoa wa Kilimanjaro.

"CCM imejitahidi kufanya siasa za chuki, lakini ukweli chama chetu kiko imara kwani kimejenga imani kubwa kwa wananchi katika kutetea maslahi yao," anasema Katibu wa Mkoa, Basil Lema.

Lema anasema licha ya hali ya siasa nchini kuwa tete kitu kinacchosababisha baadhi ya wagombea katika baadhi ya maeneo kuogopa kusimama, lakini wameendelea na uhamasishaji na maeneo yote ya mkoa huo, wanagombea.

"Hakuna sehemu mgombea wa CCM atakayepita bila kupingwa kwani tumejipanga na tutashinda kwa kishindo kikubwa,"

### WANACHAMA

Elisante Munuo ni mwanachama wa Chadema. Anasema mbali na changamoto ambazo wanakabiliana nazo yakiwamo matamko mbalimbali ya baadhi ya viongozi wa serikali na CCM, bado watafanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi wanaowataka.

"Changamoto ni nyingi lakini hatujakata tamaa, tutafanya maamuzi ambayo yataiacha CCM na baadhi ya viongozi wa serikali mdomo wazi," anasema na kuongeza:

"Tumejipanga kushinda kwa asilimia 100, viongozi tulio nao wanajitahidi na tunawaamini."

Naye Mariamu Msuya, mwanachama wa CCM anasema kutokana na jitihada za mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Dk. Magufuli za kuwatetea wanyonge na kupigania maendeleo, wagombea wengi wa CCM watapita bila kupingwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, na uchaguzi mkuu mwakani.

# Mfumo wa Iran uliowekwa Iraq, Lebanon waanza kusambaratika

• Hata Washia waisusa Hezbollah



Distributed via ippmedia

Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

KUNA viashiria kuwa nguvu ya Iran, inaanza kupungua katika eneo la Mashariki ya Kati baada ya milipuko ya kisiasa na maandamano yasiyoisha kuzikumba Iraq na Lebanon, nchi mbili ambazo mfumo wake wa kisiasa unaitegemea Iran kwa kiasi kikubwa.

Nchi zote mbili zina makundi makubwa ya kijeshi yanayopokea amri kutoka Iran, huku mfumo wa utawala na mgawo wa rasilimali unategemea makundi ya kisiasa hasa yaliyo na majeshi yanaelekezwa kutoka Iran, na wanaweza kufikia muafaka wa utawala kwa kiwango gani na makundi mengine.

Kwa kawaida mfumo huo umekuwa ukifanya kazi lakini viashiria vya kuyumba kwake vinaongezeka.

Baadhi ya wachunguzi wa habari nchini Marekani wameanza kuunda hisia mpya kwa Iran, ina uwezo mkubwa wa kushawishi makundi yanayoendana na itikadi yake kutwaa madaraka nchi moja au nyingine, lakini siyo ufanisi katika kutumia madaraka hayo.

Siyo rahisi kusema kuwa tatizo liko katika uwezo wa kutawala au kutumia vyema madaraka ya nchi, kwani taasisi za serikali nchini Lebanon zimedumu kwa takriban miaka 30 tangu kumalizika kwa vita kati ya makundi tofauti ya kiitikadi nchini humo kuanzia mwaka 1975 hadi 1990.

Ni vita ambavyo watu 120,000 walipoteza maisha, zaidi ya milioni moja wakaondoka nchini kuhamia kwingine na hasa Ulaya ya Kusini na Magharibi, mpangilio mpya wa utawala ukakubaliwa, ukadumu hadi sasa.

Badala ya kudai kuwa Iran haina uwezo wa kushikilia hatamu za utawala baada ya kupata madaraka au makundi ya itikadi hiyo kushika hatamu za nchi, ni bora kuangalia jinsi Iraq na Lebanon zinavyokumbwa na wimbi la kutoridhika hasa miongoni mwa vijana.

> Iran ni nchi inayoongozwa na itikadi ya 'wilayat e fiqh,' yaani utawala wa kuhani (mfikiriaji sheria ya dini aliye mahiri kati ya wenzake).

Kama ilivyo barani Ulaya, Amerika ya Kusini katika nchi kadhaa, Mashariki ya Mbali huko Hong Kong na barani Afrika huko Sudan, Algeria na Misri (kwa sababu tofauti kiasi) hivi karibuni, ndiyo hali inayoinyemelea Iraq na Lebanon.

Suala muhimu la kimkakati ni kama Iran inamudu kutanzua hali hiyo, wakati nafasi yake ya kufanya biashara na kuingiza mapato imebanwa na Marekani.

Kilichowashangaza wafuatiliaji wa habari ni jinsi maandamano hayo yalivyoteka miji ya Lebanon kila upande wa nchi, na siyo tu jiji la Beirut, na cha msingi ni kuwa watu hawaridhiki tena katika nafasi ambayo kila jumuiya imepangiwa katika mfumo huo.

Wachunguzi nchini Marekani wanafikia tamati kuwa kinachosambaratika hivi sasa ni uwezo wa Iran kushawishi watu wa mataifa yanayoizunguka kuwa njia yake ya kiitikadi ndiyo bora na kutii mifumo ya utawala na mgawo wa majukumu kuelekea mikakati mipana ya kiitikadi.

Ndiyo inayotawala mwenendo wa Iran tangu mapinduzi ya mwaka 1979, yanayokwamishwa na kibano cha uchumi.

Iran ilishinda katika misukosuko mikubwa ya eneo hilo hasa kuanzia kuzuka kwa Uamsho wa nchi za Kiarabu mwaka 2011 na kuuawa Osama bin Laden mwezi Mei 2011.

Ilisaidia kuzuia kuondolewa utawala wa Syria licha ya kuwa nguvu kubwa zaidi ilikuwa ni ya Russia, na nchini Lebanon na Iraq vyama na makundi ya kijeshi tiifu kwa Iran yameendelea kushinda.

Tatizo kwa upande mmoja ni kuongezeka kwa vita, vikwazo na kupauka uchumi kutokana na mzingiro huo.

Wachambuzi katika jarida muhimu la Marekani kuhusu siasa za nchi za nje wanasema kuwa kwa miongo minne tangu mapinduzi ya 1979, watawala nchini Iran wamefaulu kutumia kila mwanya kupenyeza itikadi na kuunda makundi ya kisiasa yanayomiliki silaha, kulinda uwezo wao wa kutetea nafasi zao katika maeneo hayo.

Wanasema kuwa ambacho Iran haikuwahi kufikiria ni 'visheni' au mtazamo mpana wa kukua kwa uchumi na mahusiano ya kijamii katika hali hiyo, suala ambalo kwa anayeelewa mfumo wa fikra unaotawala Iran, halina msingi halisi.

Iran ni nchi inayoongozwa na itikadi ya 'wilayat e fiqh,' yaani utawala wa kuhani (mfikiriaji sheria ya dini aliye mahiri kati ya wenzake).

Ndiye anayesimamia serikali inayoundwa na shura, yaani Baraza la Wawakilishi linalochaguliwa na umati wa watu huku kanuni za msingi za mapinduzi zikifuatwa.

Kwa maana hiyo hapakuwa na haja ya kufikiria nini kitatokea katika uchumi na baada ya hapo Iran itafanya nini, kwani kila utawala uchumi duniani hutegemea kanuni za msingi za kuendesha nchi, kwa mfano demokrasia ya vyama vingi, au soko.

Kuwapo mabadiliko ya kina au ya ghafla ni kitu kinachotokana na historia kisichoweza kubuniwa mapema, lakini uwezo wa kukabiliana na hali kama hiyo unaendana na kile kilichokuwa kinatazamiwa awali.

Kwa upande huo ni wazi kuwa matazamio ya mapinduzi ya mwaka 1979 yalikuwa ni kuendelea kupata nguvu kwa itikadi ya kimapinduzi (ya dini, si yale ya kikomunisti) na kupungua nguvu kwa 'ubeberu,' mfumo wa nchi za Magharibi wa demokrasia, soko huria na kukamata rasilimali kote duniani.

Kimsingi, Iran ilikuwa na njozi ya itikadi ya mfumo wa jamii inayoutetea kukubalika kote Mashariki ya Kati.

Kimsingi hali hiyo ilifikiwa lakini haiwezi kudumu zaidi ya miaka 40, kwani kuna mkondo mkubwa zaidi wa uchumi ina maana kwa hiyo siasa ambayo unaeleweka katika fikra tofauti ya kimapinduzi, kuwa dunia nzima inataka maisha bora zaidi, yaani bidhaa bora kwa bei rahisi.

Ndiyo inakuwa utandawazi, kuwa nchi ikiwa na viwanda vyake vya teknolojia ya zamani na madeni lukuki ya kutafuta vipuri au spea za viwanda hivyo inajilundikia madeni, walanguzi wanapenyeza bidhaa bei poa, kodi zinazidi kwani nchi haina uwezo wa kununua vitu vingi kutoka nje.

Silaha kuu ya Iran ilikuwa ni mafuta, sasa teknolojia imebadilika hata Iran hivi majuzi ilipoipiga Saudia katika medani ya mafuta, bei yake haikupanda kubadili nauli kokote.

Ambacho pia kinaitesa Iran na watu wake au washiriki wa mfumo wake katika nchi kama Iraq na Lebanon kwa karibu na kwingineko kwa njia tofauti ni kuwa kupenya kwa teknolojia za habari na mawasiliano, zimerahisisha ushawishi wa kisiasa na kuunda mifungamano ya kutoa madai, na hata kubadili serikali.

Mtafaruku uliomwangusha hayati Rais Mohamed Morsi nchini Misri ilikuwa ni Bunge la Undugu wa Kiislamu (Muslim Brotherhood) wakiwa ndiyo wengi kupitisha marekebisho ya katiba kuwa umri wa kuolewa binti iwe ni miaka kuanzia 12, kwa ruhusa ya baba yake.

Nchini Sudan maandamano yalianza bei ya mikate ilipopanda wakati tayari watu wanapata tabu kumudu maisha, na nchini Lebanon serikali ilileta kodi mpya ya matumizi ya WhatsApp, mtandao unaopendwa kutumiwa na makundi ya kijamii ili kuzuia wasiwasiliane.

Kwa upande mwingine, unaweza kusema kuwa itikadi ya utawala nchini Iran kuanzia mwaka 1979 iliegeshwa katika dhana kuwa nje ya utawala huo kuna falme za Kiarabu ambazo pia zinashirikiana na Marekani kwa kina.

Mtazamo huo umekwamishwa na kuzuka kwa Dola ya Kiislamu na mkasa wa kuuawa yeyote asiyekubaliana na kila wanachosema – tatizo ambalo pia liliigusa Iran wakati wa mapinduzi kama ilivyo kwa mapinduzi kote duniani.

Sasa hatari ya kuzuka dola ya aina hiyo inaondoa ushawishi wa hisia kuwa unaweza kuunda 'demokrasia ya kidini' kwani huwezi kutabiri nani atachukua madaraka. Vijana wanataka ajira na uhuru, basi.



# Neema yaonekana Mto Ruaha Mkuu

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

JITIHADA za kutunza vyanzo vya maji vya Mto Ruaha Mkuu zimekuwa na mafanikio makubwa mwaka huu na kushuhudia ongezeko kubwa la maji yanayoingia Bonde la Ihefu wilayani Mbarali na pia kwenye bwawa la Mtera.

Katibu wa Bodi wa Kuendeleza Bonde la Mto Rufiji, Idrisa Msuya, alisema wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa vya kutunza mazingira kwa watumiaji 35 katika bonde hilo vilivyotolewa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Vifaa hivyo ni pamoja na baiskeli, mapanga, mashoka, makwanja, miamvuli na tochi zinazotumia nishati jua kwa ajili ya kutumia nyakati za usiku. Alisema miaka ya nyuma mto huo ulikuwa unakauka na kuhatarisha maisha ya viumbe hai vinavyoishi majini na wanyamapori kwenye hifadhi ya taifa ya Ruaha pamoja na kupungua kwa uzalishaji wa umeme bwawani Mtera.

Alisema katika kituo cha Nyaluhanga kuanzia mwezi Septemba ujazo wa maji yaliyokuwa yanatiririka yalikuwa chini ya lita 100 kwa sekunde, lakini mwaka huu kiwango cha maji yanayotiririka kimefikia lita 3,000 kwa sekunde.

"Lakini miaka ya nyuma kipindi kama hiki hifadhi yetu ya Ruaha, maji yalikuwa yanakauka na wanyama waliteseke, lakini tumefuatilia na kuona maji yanatiririka vizuri," alisema Msuya.

Aidha, utunzaji wa vyanzo vya maji vya mto huo unaleta matumaini ya kufanikiwa kwa mradi mkubwa wa kufua umeme katika Mto Rufiji wa Bwawa la Nyerere (Stiglers Gorge).

Mwenyekiti wa Bodi ya Bonde la Maji ya Mto Rufiji, Vitalis Mnyanga, alizipongeza jumuiya za watumia maji wa bonde hilo kuwezesha maji kuongezeka Mto Ruaha.

Alisema Wizara ya Maji ilibaini kuwa jumuiya hizo zinafanya kazi katika mazingira magumu ndiyo maana imezisaidia vifaa vya kuboresha mazingira na kuongeza ufanisi hasa kwa wakulima.

Vifaa vilivyonunuliwa vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 140 na kuwataka kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Kila jumuiya inapata vifaa vyenye thamani ya Sh. 4,000,000, baadhi ya vifaa hivyo ni baiskeli, mapanga, mashoka, makwanja, miamvuli kwa ajili ya kujikinga na mvua na tochi za jua kwa ajili ya kutumia nyakati za usiku na tunaamini vitatatua baadhi ya matatizo," alisema Mnyanga.

Wilaya ya Mbarali ambayo ndiyo yenye vyanzo vingi vya maji, vifaa hivyo vya kusaidia kutunza mazingira vilikabidhiwa kwa jumuiya tatu za watumia maji na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya, Asher Mwakimonga.

Miaka ya hivi karibuni baadhi ya wanyama na viumbe hai walikufa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutokana na ukame hali ambayo iliyotishia ikolojia ya hifadhi hiyo.




Baadhi ya watalii wa ndani wakiangalia Ziwa Ngosi, lililopo mkoani Mbeya juzi, ambalo ni la pili kwa ukubwa barani Afrika kwa maziwa yanayotokana na mlipuko wa Volkano, ni ziwa lenye mwonekano wa kipekee kutokana na umbo lake ambalo linafanana na ramani ya Bara la Afrika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wataka udhibiti wa mbegu feki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima mkoani Mbeya wameiomba serikali kudhibiti uzalishaji na uuzaji mbegu feki ili kuepusha usambazaji mbegu duni kwa wakulima unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Wakulima hao walisema kila unapoanza msimu mpya wa kilimo, wauzaji wa pembejeo za kilimo, wanaongezeka na baadhi yao kuwauzia mbegu feki zisizoota na hata zikiota hazizai.

Walitoa ombi hilo juzi walipokuwa wanazungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambao una wafanyabiashara wengi wanaotegemewa na wakulima wa Wilaya ya Mbeya.

Mmoja wa wakulima hao, Aidan Siwila, alisema baadhi ya wafanyabiashara wanatumia nafasi ya uelewa mdogo wa wakulima wa utambuzi wa mbegu kuwauzia mbegu feki.

Aliwaomba wataalamu wa udhibiti kukagua mara kwa mara hasa kipindi hiki ili maduka yanayobainika kuuza mbegu hizo yafungiwe kuuza pembejeo hizo.

"Kila mwaka katika mkoa wetu wanakuja wakaguzi kukagua maduka ya pembejeo na wanakamata shehena za kutosha za mbegu feki. Lakini wanakuja wakati tayari tumeshapanda na wakati mwingine tunakuwa tumeshazinunua hizo hizo. Sasa mwaka huu tunawaomba wawahi kufanya ukaguzi," alisema Siwila.

Mkulima Martin Mwenizuwa, alisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kununua mbegu za mahindi na kutii maagizo ya wataalamu lakini huambulia mazao kidogo kutokana na kuuziwa mbegu feki.

Alisema katika Mji wa Mbalizi kuna baadhi ya wafanyabiashara wakubwa walikamatwa mwaka jana wakizalisha mbegu feki, lakini mpaka sasa maduka yao bado yanafanya kazi hivyo ni hatari kwa baadhi ya wakulima ambao hawayajui.

Aliwaomba wataalamu kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuzitambua na kuziepuka mbegu feki za mazao hayo na waziepuke.

# Hifadhi ya Mporoto hatarini kutoweka

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANAVIJIJI vinavyozunguka msitu wa Hifadhi ya Mporoto, iliopo jijini Mbeya na Rungwe, vimeharibu mazingira ya msitu huo na kuhatarisha hatima ya ustawi wake.

Ofisa Utalii wa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mlima Rungwe kutoka Wakala wa Usimamizi wa Misitu (TFS), Jesica Mgata, alisema wakati wa ziara ya watalii wa ndani.

Watalii hao walihusisha wanahabari na wasanii wa mkoani Mbeya zaidi ya 20 waliotembelea Ziwa Ngosi lililopo ndani ya msitu huo.

Alisema baadhi ya shughuli zinazofanywa na wananchi hao zinaharibu mazingira na kusababisha kutoweka msitu huo ndicho chanzo cha Ziwa Ngosi ambalo halina chanzo kingine.

Alizitaja baadhi ya shughuli zinazofanywa na wananchi hao kuwa ni pamoja na uwindaji haramu, uchomaji moto ovyo hasa wakati wa kiangazi ili kuandaa mashamba.

Vilevile baadhi hukata baadhi ya miti ikiwamo mianzi kwa ajili ya kujengea nyumba na kutengenezea nyungo pamoja na kuchuna mifugo.

"Tunakabiliana na uharibifu huo wa mazingira kwa njia mbalimbali, tunatoa elimu ya utunzaji wa mazingira, tunawapatia ajira za muda hasa kutengeneza mipaka na kukwatua njia za kukabiliana na moto, tunawagawia mizinga ya nyuki na miche ya miti ili waipande kwa ajili ya kuni," alisema Mgata.

Akizungumzia Ziwa Ngosi, ambalo ni la pili kwa ukubwa barani Afrika kwa maziwa yanayotokana na volkano pamoja na umbo lake kufanana na ramani ya Afrika idadi ya watalii imeanza kuongezeka na kufikia zaidi ya 700 kwa mwaka.

Alisema Wizara ya Maliasili na Utalii inatarajia kuanza utekelezaji wa mpango wa kuiondoa mimea vamizi ndani ya hifadhi ya misitu asilia ya Rungwe ukiwamo wa Mporoto.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha la Mbeya ambalo linajishughulisha na mambo mbalimbali yakiwamo uhifadhi wa mazingira na upangaji wa bajeti, Festo Sikagonamo, alisema wananchi wanahitaji elimu ya kutosha ili watunze mazingira.

Alisema Elimisha inawaelimisha wananchi namna ya kutunza vyanzo vya maji na kuepuka kufanya shughuli za kijamii kama kilimo kwenye maeneo hayo.

Aidha, wanafunzwa kupanga bajeti katika ngazi ya familia ili wapunguze matumizi ya nishati zitokanazo na miti kama mkaa na kuni.

Baadhi ya watalii waliotembelea Ziwa Ngosi waliiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara zinazoenda kwenye ziwa hilo ili iwe rahisi kwa watalii kulifikia. Mmoja wa watalii hao, Esther Mwakalobo, alisema ziwa hilo lina mwonekano wa pekee na endapo miundombinu itaboreshwa watalii wengi watatembelea na kuliingizia taifa mapato ya kutosha.





# Wasiosikia waiomba NEC wakalimani lugha ya alama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WALEMAVU wa kusikia (viziwi) wameitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuweka wakalimani wa lugha ya alama katika maeneo ya vituo vya kujiandikisha, mikutano ya kampeni na kwenye vituo vya kupigia kura ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuwachagua viongozi wao.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania (Chavita) Mkoa wa Dodoma, Yusuph Mloli, alipokuwa akichangia mada katika mkutano wa wadau wa uchaguzi kuelekea zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura mkoani Dodoma.

Mloli alisema moja kati ya changamoto ambazo wamekuwa wakikumbana nazo ni kukosekana kwa wakalimani wa lugha za alama katika vituo vya kujiandikisha, mikutano ya kampeni na wakati wa zoezi la kupiga kura.

"Tunaomba tume ya Taifa ya Uchaguzi iangalie namna ya kuweka wakalimani wa lugha ya alama katika maeneo mbalimbali ili na sisi tuweze kushiriki kikamilifu katika kuchagua viongozi wetu," alisema Mloli.

Aidha, alisema wanashindwa kushiriki hata mikutano ya kampeni za wagombea katika chaguzi ambazo zimekuwa zikifanyika nchini kutokana na kukosa wakalimani.

"Kutokana na kukosa wakalimani kwenye mikutano ya kampeni, tunashindwa hata kuchagua viongozi wenye sifa kutokana na kushindwa kuzielewa sera zao, hali ambayo inatulazimu kusaidiwa kuchaguliwa kiongozi na watu wengine kwa mujibu wa utashi wao," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu (Shivyawata) mkoani Dodoma, Jastus Ng'wantalima, alisema kuwa moja ya changamoto kwa watu wenye ulemavu katika mikutano ya kampeni ni uwapo wa vurugu katika maeneo mbalimbali.

Ng'wantalima alisema kutokana na hali hiyo, walemavu wengi wamekuwa wakikosa fursa ya kushiriki katika mikutano ya kampeni kwa kuhofia usalama wao.

Akijibu hoja hizo, Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, alisema suala la kufanya vurugu katika mikutano ya kampeni ni uhalifu kama yalivyo makosa mengine.

"Kutokana na hali hiyo sisi kama tume huwa tuna utaratibu wa kukutana na vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na vyama vya siasa kujadiliana namna ya kuwa na uchaguzi wenye amani, lakini huru na wa haki," alisema Jaji Kaijage.



Mkurungenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi (kulia), akimkabidhi cheti, Sebastian Ollomy, baada ya kushiriki mafunzo ya mawakala wa Benki ya NMB, Mkoa wa Dodoma yaliyofanyika mwisho wa wiki jijini humo. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 14/- zakopesha pembejeo wakulima wa mahindi 52,000

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ZAIDI ya Sh. bilioni 14 zimetumika kwa ajili ya mradi wa utoaji mkopo wa pembejeo za kilimo cha mahindi kwa wakulima zaidi ya 52,000 waliojiandikisha kupata mkopo huo kwenye msimu wa kilimo uliyopita katika mikoa mitano.

Hayo yalibainishwa jijini Dodoma na Ofisa Mawasiliano wa taasisi isiyo ya kiserikali ya One Acre Fund (OAF), Dorcas Tinga, alipokuwa akizungumza na gazeti hili.

Tinga alisema lengo la mkopo huo ni kuhakikisha wanainua kilimo cha mahindi kwa kuwafanya wakulima kulima kwa tija, na kuinua vipato vyao tofauti na ilivyokuwa awali ambapo wakulima wengi walikuwa wanalima bila tija na kushindwa kufikia malengo. Akizungumzia changamoto ya wakulima kushindwa kutumia kwa usahihi viuatilifu, Tinga alisema kwa sasa hawana mradi huo, lakini siku za usoni wanaweza kuifanyia kazi changamoto hiyo kwa undani zaidi ili kulinda afya za wakulima na kuongeza uzalishaji mali wa wakulima nchini. Alisema katika misimu miwili iliyopita ya mwaka 201718, walitoa elimu ya viuatilifu kufuatia kuzuka kwa ugonjwa wa viwavi jeshi kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hivyo kutoa elimu hiyo kwa wakulima ili kunusuru mazao kuliwa na wadudu hao.

Alisema mkopo huo unatolewa kwa kikundi cha wakulima kuanzia watano hadi 16, ambao hupewa kifurushi kamili cha mbolea za kupandia na kuvunia na mbegu kulingana na ukubwa wa shamba lake, mkopo ambao mkulima ataulipa kwa fedha baada ya msimu wa mavuno kukamilika. Alisema baada ya mkopo huo maofisa shamba hutoa mafunzo ya namna ya kuandaa shamba, palizi, matumizi sahihi ya mbolea na namna ya kuvuna ili kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo chao. Tinga aliitaja mikoa ambayo imefikiwa na fursa hizo ni Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Arusha.

# Mufti ahimiza Waislamu elimu ya Tehama

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MUFTI wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, wamewata mashekhe, maimamu, walimu na waumini wa dini ya Kiislamu kujiunga kwenye mafunzo ya elimu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo yameandaliwa na ofisi yake kupitia Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata).

Kwa hivi sasa mafunzo hayo yanaratibiwa na Bakwata ambayo yanatolewa kwa miaka mitatu 2019-21 na yatagharimu takribani Sh. bilioni 1.4 na yamepangwa kuifikia mikoa 26 ifikapo Juni 2020. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa madarasa ya IT na lugha mbalimbali jijini hapa, Mufti Zuberi, alisema kuwa Waislamu wanatakiwa kujiendeleza na ili waweze kubadilika kupitia mafunzo ya Tehama kupitia kompyuta kwa hivi sasa. Alisema pamoja na waumini wa dini hiyo kufahamu vizuri zaidi elimu ya kurani, lakini kwa hivi sasa pia ni wakati wake kwa mashekhe, maustadhi, maimamu na walimu wa madarasa nchini, kujikita kwenye mafunzo ya elimu hiyo.

"Madarasa hayo yatakayofunguliwa katika maeneo mbalimbali nchini yatakuwa katika taasisi mbalimbali za Kiislamu, vituo vya elimu, madrasa na shule za sekondari za Kiislamu, ili Waislamu wengi wapate nafasi ya kutumia vituo hivyo kujifunza elimu hiyo," alisema.

Alisema wakati umefika kwa Waislamu kujifunza elimu ya mazingira ili kuelewa elimu ya sayansi ambayo pia imeandikwa ndani ya Koran, hivyo wasiache elimu hiyo wajifunze ili kwenda sambamba na maendeleo ya dunia.

Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Shaban, alipongeza mkakati wa Mufti wa kurekebisha mambo mbalimbali katika Bakwata na hasa kupigania maendeleo ya chombo hicho hususani kwa kuanzisha mradi huo wa mafunzo.

Alisema kutokana na kazi nzuri anazofanya alistahili kuwa Mufti wa Afrika Mashariki kwani hata nchi za nje wanasema angestahili kushika nafasi hiyo kutokana na umahiri wake wa kuijenga Bakwata na Uislamu kwa ujumla.

Mratibu wa Mafunzo hayo ya Tehema na Lugha kutoka Ofisi ya Mufti, Sheikh Harith Nkussa, alisema mafunzo hayo yanalenga kusaidia vijana na Watanzania kwa ujumla ili kukabiliana na changamoto za kielimu na kiuchumi za ulimwengu wa kidigitali na kielektroniki.

"Mafunzo hayo yanawahusu wanafunzi waliohitimu kidato cha nne na kukosa ajira, mashehe, maustadhi na walimu wa madrasa ili kuongeza ujuzi katika elimu ya kompyuta," alisema.

Nkussa alisema masomo hayo yatamwezesha mtahiniwa kujiajiri au kuajiriwa kwa haraka na popote nchini kwa pato la faida kubwa.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa katika Chuo cha Ualimu cha Al-haramain jijini Dar es Salaam ambapo zaidi ya masheikh 450 wamepata mafunzo.

Chuo hicho kinatoa mafunzo katika ngazi ya cheti na mwakani kitaanza kutoa Diploma, ambapo walimu watakaohitimu watakuwa wakitoa mafunzo katika vituo mbalimbali nchini.

Uzinduzi wa madrasa ya mafunzo ya Tehama na Lugha yamefanyika jijini Dar es Salaam katika vituo viwili, mkoani Njombe, Arusha, Kilimanjaro na sasa Dodoma na wataenda pia Singida na mwakani watakamilisha mikoa 26.





## Mwakilishi azimwagia maskani mabati, jezi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WANACHAMA wa CCM katika maskani nane za Chama Cha Mapinduzi zilizomo katika jimbo la Jang'ombe, wamenufaika na vifaa mbalimbali vilivyotolewa na mwakilishi wao ikiwa ni utekelezaji wa ahadi zake kwa wapiga kura wake.

Mwakilishi wa jimbo la Jang'ombe Ramadhan Hamza Chande, alitoa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 1.5 kwa maskani nane za Chama Cha Mapinduzi zilizomo katika jimbo hilo.

Akizungumza katika mwendelezo wa ziara zake katika maskani mbali mbali za CCM jimboni humo, Chande alisema kuwa vifaa hivyo ambavyo ni mabati ya kuezekea nyumba, jezi za mpira wa miguu na fedha taslimu ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi zake alizowaahidi wananchi katika kampeni za uchaguzi zilizopita.

Alisema katika uongozi wake ndani ya jimbo hilo ataendelea kuwa karibu na wananchi wa makundi yote, bila kuwabagua kwani kila mmoja ana umuhimu wake katika maisha ya kisiasa.

Katika maelezo yake mwakilishi huyo aliwambia viongozi na makada wa maskani hizo kuwa Chama Cha Mapinduzi kinawathamini kutokana na mchango wao wa kuimarisha taasisi hiyo kisiasa na kiuchumi.

Katika ziara hiyo aliwakumbusha wananchi hasa wanachama wa CCM kuhakiki vitambulisho vyao vya Mzanzibari mkaazi sambamba na kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura ili wapate uhalali kukipigia kura Chama Cha Mapinduzi na kukipa ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Diwani wa wadi ya Kwaalinatu Fatma Suleiman Juma, aliwataka wananchi kuendelea kujali na kuitunza miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali ya CCM ili idumu kwa muda mrefu kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Akizungumza katika shughuli hiyo, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo, Ali Hamad Ibrahim, alisema ziara hiyo imeongeza hamasa kubwa kwa wana maskani hao kwani changamoto zao za muda mrefu zimetafutiwa ufumbuzi wa kudumu na mwakilishi huyo.

Aliongeza kuwa kila mwanachama na viongozi wa CCM ndani ya jimbo hilo anatakiwa kuandaa vizuri zana zake za mapambano ya vita ya kisiasa kuelekea uchaguzi wa 2020, kwani muda wa kusema kwa maneno umepita na kilichobaki ni kutekeleza kwa vitendo.

# Wananchi kufuatilia uchaguzi kieletroniki

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imetoa namba itakayowawezesha wananchi popote walipo -mijini au vijijini kupiga simu na kujua taarifa zote zinazohusu uchaguzi.

ZEC inachukua hatua hiyo katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata urahisi wa kujua taarifa za kiuchaguzi hasa kuandikishwa, kitambulisho cha Mzanzibari mkazi na kituo cha kupigia kura.

Hayo yalielezwa na Ofisa Habari na Uhusiano wa ZEC Jaala Makame Haji, jana mjini Zanzibar. Alisema mwananchi anayetaka kujua kituo chake cha kupigia kura na kuhakiki taarifa za upigaji kura , atapiga simu kwenye namba hizo na kupata maelezo. Alizitaja namba hizo kuwa ni *152*29# (nyota mia moja hamsini na mbili, nyota mbili tisa, alama ya reli) ambayo itamwezesha pia mwananchi kujua kama kitambulisho chake cha Mzanzibari mkazi kimehakikiwa ama hakikuhakikiwa.

Alisema wameweka nambari hizo kutokana na usumbufu walioupata wananchi katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2015 na wengine kulazimika kuingia katika tovuti ya ZEC huku baadhi ya wananchi wakishindwa kwani hawana elimu ya masuala ya mtandao.

Aidha, wengine walishindwa kwa sababu hawamiliki simu janja zenye intanet.

"Siyo wananchi wote ambao wanajua kuingia katika mitandao na kupata taarifa za uchaguzi. Kwasababu si wote wanaoishi kwenye miundombinu yenye huduma hizo. Wapo wanaoishi vijijini wao wanategemea zaidi kupata taarifa katika vyombo vya habari na simu zao za mikononi ndiyo maana ZEC imeona ipo haya ya kuweka namba hiyo maalum ambayo mwananchi anaweza kupata taarifa zote za uchaguzi na akafahamu kile anachotamani."Alisema ofisa huyo. Aidha, kuwapo kwa namba hiyo maalum ya kupata taarifa za uchaguzi kutawasaidia wananchi kupata maelezo sahihi yanayotolewa na tume na kuachana na taarifa za upotoshaji zinazotolewa na vyanzo visivyo rasmi.

Haji aliwataka wananchi kutumia namba hiyo kwaajili ya taarifa zinazohusu masuala ya uchaguzi na si kuuliza maswali ambayo hayahusiani na madhumuni yaliyowekwa.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akipokea Kitambulisho kipya cha Kielektroniki cha Mzanzibar Mkaazi kama ishara ya Uzinduzi rasmi wa Vitambulisho hivyo, kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maluum za SMZ, Haji Omar Kheir , wakati wa hafla iliofanyika Kikwajuni Mjini Zanzibar jana.
**PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Taarifa za wanajamii zitadhibiti mihadarati

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Mjini, Marina Joel Thomas , amewataka wananchi kutoa taarifa na kushirikiana na jeshi la polisi na viongozi waliopo wa shehia zao ili kuwanasa wanauza dawa za kulevya.

Alisema ni lazima wafanye hivyo katika kuendeleza juhudi za kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na biashara haramu ya dawa hizo katika maeneo yao.

Tomas aliyasema hayo katika mkutano uliojumuisha kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Mjini, kitengo cha kupambana na dawa za kulevya pamoja na wananchi wa shehia za Kundemba, Makadara na Mwembeladu.

Alisema vijana wanaangamizwa na utumiaji wa dawa za kulevya huku baadhi ya wananchi wanaowajua wahusika, wakiacha kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola juu ya wauzaji wa dawa hizo waliopo katika shehia zao.

Alisema jambo hilo linasababisha taifa kuendelea kupoteza vijana kwa matumizi ya dawa hizo.

Alisema wananchi kwa pamoja wana jukumu la kushirikiana na jeshi la polisi katika kuwafichua wauzaji wa dawa hizo katika maeneo yao ili kuwanusuru vijana ambao tayari wameshaingia kwenye utumiaji wa dawa hizo na hata wale ambao hawajaingia ili wasizitumie.

Ofisa wa Polisi kutoka makao makuu ya polisi Zanzibar, Omar Khamis Abdallah, aliitaka jamii kushirikiana kwa karibu na jeshi hilo kukemea na kupambana dhidi ya matumizi na uuzaji wa dawa za kulevya katika maeneo yanayowazunguka ili kuokoa nguvu kazi ya taifa.

Alisema inasikitisha kuona baadhi ya wazazi wanashindwa kuwakemea vijana wanaotumia dawa hizo huku wakichukulia biashara hiyo kama ni jambo la kawaida na kusababisha kuongezeka kwa wimbi kubwa la vijana kujiingiza katika biashara hiyo siku hadi siku.

Katika mkutano huo Mkurugenzi Mdhibiti na Uchunguzi kutoka Tume ya Dawa za Kulevya Juma Abdulrahman , alisema serikali imeamua kwa makusudi kupambana na dawa za kulevya kwa kurekebisha sheria katika vifungu vya adhabu ambapo kwa sasa kifungo cha chini ni miaka isiyopungua 15.

Alisema sheria hiyo inawagusa na wale wanaoishi katika nyumba inayofanyika biashara hiyo hata kama hawahusiki katika uuzaji wa biashara hiyo haramu.

# Utekelezaji mfumo kudhibiti vikwazo vya biashara kuanza

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema itaanza kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara nchini (Blueprint) ili kurahisisha zaidi ufanyaji biashara Tanzania.

Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Geoffrey Mwambe, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mambo mbalimbali ya biashara na uwekezaji tangu kituo hicho kianzishwe.

Mwambe alisema katika ripoti ya mwaka 2019/20 ya urahisi wa ufanyaji biashara iliyotolewa na Benki ya Dunia (WB), Tanzania imeshika nafasi ya 141 kati ya nchi 190.

"Kwa mujibu wa ripoti hii ikilinganishwa na ya mwaka jana, Tanzania imepanda kutoka nafasi ya 144 hadi 141 ambapo mwaka huu tumeyazidi mataifa matatu," alisema Mwambe na kuongeza:

"Tunaamini utekelezaji wa Blueprint kama tunavyojua ni nyenzo ya kufanya marekebisho ya msingi, ripoti ijayo tunataka tupande zaidi," alisema.

Mwambe alisema zipo juhudi ambazo serikali inazifanya za kuleta mkakati mpya wa utekelezaji wa Blueprint.

"Nafikiri muda muafaka ukifika mtataarifiwa na mtaona, namna ya utekelezaji iliyokuwa ikifikiriwa mwanzo siyo sahihi, itafika muda muafaka mamlaka inayohusika itatoa taarifa, lakini kama kituo tunashirikishwa," alisema.

Alisema watahakikisha Blueprint inatekelezwa kwa haraka zaidi ili kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa juu katika kuvutia uwekezaji na biashara.

Pia, alisema lengo la serikali ni kupanda hadi kufika kwenye nafasi ya nchi 100 ya nchi zenye urahisi wa ufanyaji biashara duniani.

Mwambe alitaja baadhi ya maeneo ambayo ripoti hiyo imeainisha Tanzania imefanya vizuri kuwa ni maamuzi ya kulinda zabuni ambayo huchukua siku 18, mazingira ya uanzishaji biashara, vibali vya ujenzi, urahisi wa kulipa kodi.

Kwa upande wa maeneo ambayo imefanya vibaya, Mwambe aliyataja ni uunganishaji wa umeme, mikopo, namna mikataba inaheshimiwa na kulindwa na usajili wa mali.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, vilitajwa vikwazo 12 vya ufanyaji biashara Tanzania, lakini imeonyesha imeboresha baadhi ya mambo kiasi ya kuifanya kushika nafasi hiyo ya 141 kati ya 190.

Maboresho hayo yameifanya Tanzania kushika nafasi ya nne katika nchi za Afrika Mashariki baada ya Rwanda, Kenya na Uganda.

Katika hatua nyingine, Mwambe alisema katika kipindi cha robo tatu ya mwaka kilichoanzia Februari hadi Septemba, TIC imesajili jumla ya miradi 227 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni mbili.

Mwambe alisema kati ya miradi hiyo, ipo ambayo utekelezaji wake utachangia ajira kwa vijana zaidi ya 38,000.

"Robo tatu hiyo ya mwaka imegawanyika mara tatu ambapo ni Februari hadi Machi, Aprili hadi Juni na Julai na Septemba. Katika miradi yote 227 iliyosajiliwa, viwanda vimeongoza kwa kusajili miradi 128, ambapo inafuatiwa na usafirishaji miradi 29," alisema.

"Miradi iliyosajiliwa ya biashara ya huduma ni 18, kilimo 15, utalii 14, uwekezaji wa majengo ya biashara miradi 10, uwekezaji wa vyuo miradi sita, uzalishaji umeme wa jua, upepo miradi miwili," alisema.




Kaimu Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (katikati), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi na Meneja wa Mastercard Afrika Mashariki, Frank Molla, kuhusu jinsi ya kulipia kwa Tigo Pesa Mastercard QR, katika hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Malipo, Mshana Mshana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC awawashia moto wabadhirifu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, ameonya kuwa yeyote aliyefanya ubadhirifu wa fedha za umma kwa kula au kutumia vibaya kwa matumizi yasiyozingatia utaratibu wa serikali, ni vyema akarudisha fedha hizo mara moja kwa hiari.

Aidha, amewataka wahusika kumwonesha nakala ya risiti ya urejeshwaji, vinginevyo atakayekiuka hatabaki salama hata kama amehama mkoa, kutoroka au kwenda kwingineko.

Alitoa onyo hilo wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na Mji Mdogo wa Ifakara, baada ya vikao vya ndani na watendaji na viongozi ikiwamo kamati za ulinzi na usalama za mkoa na wilaya na baadaye wakuu wa idara na madiwani wanaounda kamati mbalimbali ikiwamo ya fedha.

Sanare alisema watumishi waliotumia vibaya fedha hizo na kushindwa kuzirudisha hatasita kuwachukulia hatua kwani serikali ina mkono mrefu kumfikia.

"Mnageuza hizi fedha za umma kama shamba la bibi, kuna huyu (anamtaja jina), amekimbia na fedha za Halmashauri ya Mji Mdogo wa Ifakara zaidi ya Sh. milioni 146, huwezi kula hela za serikali ovyo ovyo na kukimbia, lazima ukamatwe na urudishe fedha hizi, OCD, RPC nataka kuona RB yake na kumsaka alipo mumchukulie hatua, vinginevyo nyie mtakuwa wa kwanza kuwajibika," alisema mkuu. Alirejea kuwataja watumishi mbalimbali wa Halmashauri ya Ifakara Mji na Kilombero waliotuhumiwa kutumia fedha za halmashauri, kula fedha au kupoteza kwa namna yeyote ile, kinyume cha taratibu, ambao waliibuliwa wakati wa ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuhakikisha wana risiti za kuonyesha kuwa wameshairejesha fedha hizo na kuambatanisha na risiti, vinginevyo waondoke kabla ya kuondolewa. "Nataka kuona yale maagizo ya Waziri Mkuu aliyekuwa Morogoro karibuni ikiwamo katika halmashauri hizi na kuagiza waliokula fedha au kutumia vibaya wazirejeshe kama wametekelezwa, hata kama hizi fedha ulitumia kihalali, kama hukufuata taratibu za serikali kinyume cha matumizi ya fedha za serikali ni lazima uzirejeshe," alisisitiza Sanare.

## Halmashauri Shy kuhama Jumatatu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Shinyanga, inatarajia kuhamia rasmi kwenye makao yake makuu katika Kata ya Iselamagazi kutoka Shinyanga Mjini, mahali ambapo ilikuwa ikitolea huduma kwa wananchi.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la halmashauri zote nchini zihamie kwenye maeneo yao.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Edward Maduhu, kuwa wameshajipanga kutekeleza agizo hilo, na kwamba wataanza kufungasha mizigo yao kuanzia Jumamosi hadi Jumapili kisha kuhama rasmi Jumatatu.

Alisema licha ya kuhamia huko, lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa majengo ya ofisi pamoja na nyumba za watumishi, hali ambayo itaathiri utendaji wao wa kazi, huku akioomba serikali kuwapatia Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kujenga majengo ya ofisi.

"Sasa hivi tunakwenda kujibana hivyo hivyo kwenye majengo ya serikali yaliyopo kwenye Kata ya Iselamagazi, ambapo ndipo makao yetu makuu. Majengo yaliyopo ni machache na hayawezi kukidhi mahitaji, lakini hatuna namna itatubidi tukafanye kazi hivyo hivyo," alisema Maduhu.

"Changamoto nyingine ni ukosefu wa nyumba za watumishi, lakini tumekubaliana hakuna mtumishi kuishi Shinyanga Mjini... wote tutakaa huko huko vijijini, ila shida hakuna hata nyumba za kupanga za kutosha, lakini baadhi wamepata wengine ndiyo bado wanahangaika," aliongeza.

Baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo ambao hawakuta kutajwa majina yao, walisema agizo hilo la halmashauri kuhamia kwenye maeneo yao lilipaswa kupewa muda mrefu, ili wajipange namna watakavyoishi huko pamoja na kujengwa baadhi ya majengo ya ofisi, tofauti na hivi sasa watakwenda kuishi maisha ya shida.

Hata hivyo, baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo ambao wanaishi maeneo hayo ya vijijini akiwamo Moyo Gondo, walipongeza halmashauri hiyo kuhamia kwenye makao yake makuu na kubainisha walikuwa wakipata shida sana kwenda mjini kwenye vikao ikiwamo na kutumia gharama kubwa za usafiri.

Mkazi wa Shinyanga Vijijini, Faustine Sengerema, ambaye anaishi Iselamagazi, alisema wamejipanga vyema kuwapokea watumishi hao pamoja na kuwapatia makazi kutokana na kusogezewa huduma karibu.

# TANGAZO

# TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/09/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Mwaka ya /Mwaka wa 30/09/2019 | Mwaka/Uliopita 30/06/2019 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 195,287 | 93,177 |
| 2. | Salio katika benki kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 568,118 | 369,649 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 2,470,912 | 2,520,157 |
| 12 | Mali nyingine | 237,300 | 299,536 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 175,387 | 180,945 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | 3,647,004 | 3,463,464 |
| | | - | - |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 1,073,627 | 815,773 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | | |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 158,479 | 172,564 |
| 28 | Madeni | 202,379 | 232,703 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,434,485** | **1,221,040** |
| **30** | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **2,212,519** | **2,242,424** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 4,493,394 | 4,487,402 |
| 32 | Akiba ya mtaji | (2,410,480) | (2,410,744) |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (16,863) | (4,100) |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 130,624 | 154,021 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 15,844 | 15,845 |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| **37** | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,212,519** | **2,242,424** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 186,203 | 132,753 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 64,428 | 56,765 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 61% | 65% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 8% | 5.3% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 230% | 309% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 68% | 73% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 83% | 83% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 32% | 82% |
| (vii) | Ongezeko la mali | 5% | 12% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO INAYOISHIA 30/09/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo ya mwaka wa sasa 30/09/2019 | Robo ya mwaka linganishi(Mwaka uliopita ) 30/09/2018 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/09/2019 | Limbikizo la mwaka linganisha (mwaka uliopita) 30/09/2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato yariba | 98,249 | 109,606 | 342,989 | 281,250 |
| 2. | Gharama za riba | (1,801) | (8,905) | (9,242) | (42,197) |
| 3. | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **96,448** | **100,701** | **333,747** | **239,053** |
| 4. | Madeni viza yaliyopitwa | | | | |
| 5. | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | (7,662) | 7,057 | (7,369) | (9,410) |
| **6.** | **Mapato yasiyo ya riba** | **63,072** | **68,985** | **129,863** | **276,547** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 63,072 | 68,985 | 129,863 | 276,547 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | - | - | - | - |
| **7.** | **Gharama zisizo na riba** | **(164,622)** | **(172,794)** | **(473,104)** | **(481,158)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (87,664) | (90,299) | (251,192) | (236,815) |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (76,958) | (82,495) | (221,912) | (244,343) |
| 8. | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **(12,764)** | **3,949** | **(16,863)** | **25,032** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | - | (1,185) | - | (7,510) |
| **10** | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(12,764)** | **2,764** | **(16,863)** | **17,522** |
| **#** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| **#** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 15 | 15 | 15 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (2.84) | 0 | (4) | 1 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | - | - | - | - |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.3% | 0.1% | -0.5% | 0.6% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wana | -0.6% | 0% | -1% | 1% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 103% | 102% | 102% | 93% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozal | 6% | 4% | 22% | 9% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30/09/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/09/2019 | Robo Mwaka iliyopita 30/06/2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2019 | Limbikizo la mwaka Linganishi(Mwaka Uliopita) 30/09/2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (16,863) | (4,100) | 22,245 | 25,032 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya: | 4,099 | (1,840) | 419 | (26,097) |
| | - Hasara Katika Mali | 5,823 | 8,293 | 21,441 | 49,098 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 49,245 | 93,264 | 476,876 | (785,786) |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| | - Mabasiliko halisi katika amana | 257,854 | (1,167,512) | (19,030) | (3,075,799) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (14,085) | (268,671) | (159,642) | 90,613 |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 62,235 | 66,418 | (23,664) | 133,512 |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | - |
| | - Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji** | **348,308** | **(1,274,148)** | **318,645** | **(3,589,427)** |
| **II:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - | - | |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | - | (16,064) | (19,411) | (44,279) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | | | - | |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | 0 | 0 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | |
| | Mengineyo (Bainisha) | | | - | 0 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **-** | **(16,064)** | **(19,411)** | **(44,279)** |
| **III:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 5,992 | (13,705) | (4,963) | 3,383,182 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslilmu | - | - | - | |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | (30,324) | (30,424) | (581,085) | (709,613) |
| | Mengnineyo | (23,397) | (90,106) | (125,804) | (68,225) |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(47,729)** | **(134,235)** | **(711,852)** | **2,605,344** |
| **IV:** | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslilmu | 300,579 | (1,424,447) | (412,618) | (1,028,362) |
| | Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/Mwaka | 462,825 | 1,887,272 | 3,526,118 | 4,052,233 |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/Mwaka** | **763,404** | **462,825** | **3,113,500** | **3,023,871** |

Distributed via ippmedia

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 30/09/2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa | 4,487,402 | 0 | -2,414,844 | 12,116 | 15,845 | 141,905 | 2,242,424 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | -16,863 | | | | -16,863 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 5,992 | | 0 | | 0 | | 5,992 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 0 | 0 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 0 | | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | | | 4,363 | | 0 | -23,397 | -19,034 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4,493,394 | 0 | -2,427,344 | 12,116 | 15,845 | 118,508 | 2,212,519 |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | 4,501,108 | 0 | -2,317,588 | 12,116 | 15,845 | 133,541 | 2,345,022 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | -4,100 | | | | -4,100 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | -13,706 | | 0 | | 0 | | -13,706 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 0 | 0 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 0 | | 0 | 8,364 | 8,364 |
| Mengineyo | | | -93,156 | | 0 | 0 | -93,156 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4,487,402 | 0 | -2,414,844 | 12,116 | 15,845 | 141,905 | 2,242,424 |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha ,sera za uandaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| | | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Mugwagi Steven<br>**Mtendaji Mkuu** | imesainiwa | 30/10/19 |
| Anthony Bichakila<br>**Mkuu wa fedha** | imesainiwa | 30/10/19 |

**Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.**

| | | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Said Msomoka<br>Mwenyekiti wa bodi | imesainiwa | 30/10/19 |
| Juma Namuna<br>Mjumbe wa bodi | imesainiwa | 30/10/19 |

215488202

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MCHANGANYIKO

**LAND CRUISER INAUZWA TOYOTA LANDCRUISER VX AMAZON, DIESEL, AUTOMATIC, INATEMBEA IPO KWENYE HALI NZURI. TSHS 24.5 Milioni. 0719 774 474.**

### VIWANJA / MASHAMBA


**SHAMBA LINAUZWA**
Shamba la Ekari 13 linauzwa liko Mlandizi barabara iendayo Bagamoyo, lina miti ya matunda inayozaa, lina umeme. Lina maji ya DAWASCO na maji ni matamu. Pia kuna kisima kirefu. Kwa mawasiliano piga simu namba 0655 099825 / 0767 237404 / 0715 237404.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA

BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA CHETI



**ALVIN M. GEORGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1619-0098 kilichotolewa na VICTORY SEKONDARI mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/KIJ/RB/423814/2019.

215485802

### KUPOTEA KWA CHETI




**DANIEL JOHN PETRO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0744/0050 kilichotolewa na NANGA SEKONDARI mwaka 2005.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**IGU/IR/170/2008.**

215485802

### KUPOTEA KWA CHETI



**SHUKURU A. BASTA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1344/0113 kilichotolewa na MWL J.K. NYERERE mwaka 2016.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi:**
**SON/TUN/RB/188893/2019.**

115487102

### KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI NA PIKIPIKI

ALLY AHMED ABDURAHMAN anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili T 259 AKM, T 268 AKM, T 272 AKM, T 284 AKM, T 288 AKM, T 294 AKM, T 300 AKM, T 449 AKM, T 464 AKM, T 473 AKM, T478 AKM, T 483 AKM, T490 AKM, T 493 AKM, T 498 AKM, T 506 AKM, T 526 AKM, T 544 AKM, T 546 AKM, T 547 AKM, T 550 AKM, T 555 AKM, T 557 AKM, T 563 AKM, T 568 AKM, T 573 AKM, T 580 T, T 586 AKM, T 625 AKQ, T 631 AKQ, T 639 AKQ,, T 240 AVJ, MC 707 ALP, T 959 AZS, T 966 AZS, T 970 AZS, T 567 BCS.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

**TAN/TAN/RB/406639/2019.**

115487602


### KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ALLY AHMED ABDURAHMAN** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili T 378 AGG, T 410 AGG, T 429 AGG, T 453 AGG, T 473 AGG, T455 AKL, T458 AKL, T 460 AKL, T 467 AKL, T 474 AKL, T 476 AKL, T 481 AKL, T 483 AKL, T 568 AKL, T 621 AKL, T 627 AKL, T 155 AKM, T 168 AKM, T 171 AKM, T 174 AKM, T 188 AKM.
Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
TAN/TAN/RB/406635/2019.

115487602

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ADONIS ALEX MLINDWA** anatangaza kupotelewa na Result Slip yenye index namba S.0473/0531 iliyotolewa na KANYIGO SEKONDARI mwaka 2019.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/MBA/RB/415023/2019.

215487502


**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa**
**Kutangaza Nasi**
**Kwa Bei Poa**
**Tupigie**
**0767 223311**



Distributed via ippmedia



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MADRID WAJIANDAA KUMCHUKUA POGBA




**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kwamba, inajiandaa kutoa ofa kwa Manchester United wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari ili kumsajili Paul Pogba, kwa mujibu wa ESPN.

Imeripotiwa kwamba, Real Madrid wanapanga kutoa kiasi cha pauni milioni 129 kwa ajili ya kumsajili kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Hivi karibuni staa huyo alikutana na Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane jijini Dubai na kuzua gumzo kubwa katika vyombo vya habari mbalimbali barani Ulaya na sasa inadaiwa Madrid wanataka kurudi kwake tena Januari.

United wanaweza kulazimika kumuuza Pogba baada ya staa huyo kuwaambia wazi hana mpango wa kusaini mkataba mwingine klabuni hapo pindi huu wa sasa utakapomalizika Juni 2021 na endapo atashindwa kufanya hivyo sasa, thamani yake itaanza kushuka.

Kwa muda sasa Pogba amekuwa nje ya uwanja kutokana na majeraha na hata akirudi uwanjani akili yake ni kufikiria tu kuondoka United dirisha lijalo la usajili Ulaya.

Distributed via ippmedia

## Costa anafurahia benchi Morata akiwika- Simeone

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesema Diego Costa ana furaha kuona Alvaro Morata amerudi kwenye kiwago chake pale Atletico Madrid licha ya kupoteza nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

Morata aliingia akitokea benchi na kufunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Bayer Leverkusen kwenye Ligi ya Mabingwa Jumanne na pia alifunga la pili Jumamosi wakati wakiwafunga 2-0 Athletic Bilbao kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania.

Wakati Morata akionekana kuzidi kujiamini, Costa anaonekana kutokuwa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mara moja msimu huu na alikuwa benchi kwenye mchezo wa mwishoni mwa wiki pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

Hata hivyo, Simeone amekanusha taarifa kwamba Costa amekasirishwa na kitendo cha kuwekwa benchi na Morata.

"Anaonekana ana furaha kwamba, Morata anafunga na kiwango chake kuendelea kuimarika," bosi huyo wa Atletico alisema akiwaambia waandishi wa habari juzi, Jumatatu.

"Ni wachezaji marafiki. Tunaendelea kuwa na Costa pamoja na wachezaji wote kikosini hapa.

"Ni kawaida washambuliaji kuwa na hofu pale wanapoona mabao yanatoka kwingine. Lakini kila mmoja yupo poa tu."







## 'Van Dijk atashinda Ballon d'Or 2019'

**LIVERPOOL,** England

'DOGO' wa Liverpool, Rhian Brewster anaamini kwamba Virgil van Dijk anastahili kushinda tuzo ya Ballon D'Or 2019.

Hata hivyo, kinda huyo amesema mpizani mkubwa wa Van Dijk kwenye kushinda tuzo hiyo ni mchezaji mwenzake, Roberto Firmino.

Kinda huyo ameanza kuibukia huko kwenye kikosi cha kwanza Anfield, lakini mwenyewe anafahamu ugumu unaomkabili katika kupata nafasi ya kucheza katika timu ya kwanza ya wababe hao wanaonolewa na Mjerumani, Jurgen Klopp.


Wachezaji saba wa Liverpool wameorodheshwa kwenye kinyang'anyiro hicho cha kusaka tuzo ya Ballon d'Or, ambapo Van Dijk na Firmino wameungana na Trent Alexander-Arnold, Alisson, Mohamed Salah, Sadio Mane na Georginio Wijnaldum.

Alipoulizwa nani atashinda tuzo hiyo, Brewster alisema beki Mdachi ndiye anayestahili baada ya kile alichokifanya na anachoendelea kukifanya kwenye kikosi hicho cha Merseyside.

"Kwa nini beki wa kati asishinde Ballon d'Or?," alisema Brewster na kuongeza naamini ni wakati wake na ana nafasi kubwa zaidi ya kuibeba.

"Watu watasema ameibadili Liverpool na hakika amekuwa akitusaidia kucheza mechi bila ya kuruhusu wavu wetu kuguswa. Nadhani Van Dijk atashinda."

## HABARI MICHEZO




# KEITA: KLOPP HABEBI MCHEZAJI LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

KIUNGO wa Liverpool, Naby Keita amesema kocha Jurgen Klopp hana mchezaji yeyote anayempendelea kwenye klabu hiyo.

Keita bado hajapenya kwenye kikosi cha kwanza cha Klopp tangu alipotua hapo akitokea RB Leipzig mwaka 2018.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea, ambaye muda wake hapo kwenye dimba la Anfield umekumbwa na majeruhi ya mara kwa mara, amebainisha jinsi kocha huyo anavyowachukulia wachezaji wenzake nyuma ya pazia.

"Sifikirii kama ana mchezaji anayempendelea zaidi au kuwa na mmoja muhimu zaidi kwake, anawasiliana na kila mtu kiuwazi tu," alisema Keita akiiambia Sky Sports News.

"Anapenda kucheza na kutania, ana mahusiano ya kimajukumu na wachezaji wote kikosini."

Alipoulizwa kama Sadio Mane ni mchezaji anayependelewa zaidi na Klopp, Keita alicheka na kujibu: "Kama nikifikia kiwango cha Mo na Sadio pengine nitakuwa napendelewa zaidi siku moja."

Liverpool ambayo haijafungwa kwenye mchezo wowote tangu kuanza kwa ligi hiyo, inaongoza msimamo wa ligi kwa tofauti ya pointi sita dhidi ya mabingwa watetezi, Manchester City kwenye msimamo wa ligi.

Distributed via ippmedia




# Bellerin ataka umoja Arsenal

**LONDON,** England

HECTOR Bellerin ameitaka Arsenal kuwa na umoja bada ya kutokea kuzozana kati ya mashabiki na Granit Xhaka wakati 'Washika Bundiki' hao wa London wakitoka sare na Crystal Palace, Jumapili.

Kikosi hicho cha kocha, Unai Emery licha ya kuongoza kwa 2-0, lakini kiliambulia sare ya mabao 2-2 na Palace pale kwenye dimba lao la nyumbani la Emirates ukiwa ni mchezo wa Ligi Kuu ya England.

Mchezo huo uliibua utata baada ya matumizi ya VAR kuwazawadia wageni penalti huku pia bao la dakika za majeruhi ya Sokratis Papastathopoulos likikataliwa.

Wakati Xhaka ambaye ni nahodha wa timu hiyo alipotolewa nje, mashabiki walimzoea na yeye akiwajibu kwa kuonesha ishara ya kutosikia.

Na baadaye Bellerin aliwataka mashabiki wa Arsenal kuwa na umoja kupitia mtandao wa kijamii.

"Wote ni binadamu, tuna hisia na wakati mwingine si rahisi kupambana na hali hii," aliandika.

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA HAZINA
HAZINA SAVING AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD
Madaraka Avenue, P.O.BOX 9111, Dar Es Salaam Tel: +255784 92 59 53, REG. No.DSR: 1822
Email:info@hazinasaccos.org, Website:www.hazinasaccos.org

**REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (EOI)**
**INVESTMENT OPPORTUNITIES AT HAZINA SACCOS BUSINESS CENTRE**

1. Hazina SACCOS Ltd is a registered Savings and Credit Co-operative Society whose main objective is to mobilize savings from members and in return provide credit facilities. The SACCOS was established in 1972 and registered on March 1973, at that time it was having 100 members, but now the number of members of SACCOS has increased to about 5,600. The SACCOS has members from all the Ministries and Government parastatals and corporations in Tanzania Mainland. The SACCOS run its activities in compliance with the Co-operative Societies Act, No.6 of 2013 and its regulations issued in 2015, the Hazina SACCOS Constitution and its internal policies.

2. Hazina SACCOS Ltd is determined to employ all the possibility for more growth and better performance to ensure sustainability of the institution. The action being taken in improving quality of services includes increasing shares, savings which contribute to an even faster growth in savings and loan portfolio which will in turn lead to improved profitability, liquidity and hence strengthening of the Society.

3. Hazina SACCOS owns a piece of land with approximately 22.80 acres located at Plot 7, Block F, at Njedengwain Dodoma City; about 13 Kilometers from Dodoma City Centre. The SACCOS aims to develop, over the said plot a business centre to comprise of a four star hotel, a shopping mall and office building. The plot is surrounded by tarmac roads from University of Dodoma and Morogoro road. It is neighbored by Road Fund Board, NEC, TANROAD and Arusha International Conference Centre (AICC).

4. Consistent with its objectives, the Hazina SACCOS Ltd is now seeking for eligible, competent, and reputable strategic investor(s) who can demonstrate the appropriate expertise and experience to invest in the development of the Business Centre. The Hazina SACCOS will contribute land for the project in this strategic partnership.

5. Attractive proposals will be selected and allocated parcels of land to develop and operate the developed properties through a qualification-based selection process on the EIOs submitted in response to this invitation.

6. The parcels of land that are already planned have been delineated as follows:
   A. Commercial/shopping mall;
   B. Four star hotel;
   C. Office block; and
   D. Other associated social and infrastructure facilities.

7. HazinaSACCOS now invites sealed bids for Expression of Interest (EOI) from eligible and reputable local and international investors to formally express their interest in becoming preferred investors in the development of the Hazina SACCOS Business Centre in Dodoma.

8. Interested and eligible prospective investors must provide information that will demonstrate their capability and experience to design, build, finance, operate and transfer projects of their choice by providing the following information:
   a) Company profile.
   b) Financial information.
   c) Average annual turnover.
   d) Legal capacity to enter into an agreement in accordance with and as is required by law.
   e) Demonstration of the ability to mobilize resources in undertaking of real estate development projects.
   a) Demonstration of expertise and skills in undertaking real estate and related infrastructure development projects.
   b) Demonstration of relevant experience in undertaking real estate development projects of similar size and scope.
   c) Demonstration of creativity to incorporate new housing development technologies.

9. Interested eligible local and international investors may submit their bids as individual or company or as a consortium of two or more individual/companies.

10. Interested local and international investors may seek clarification in writing, and the same to be received, at least fourteen (14) working days (Mondays to Fridays) before the date of closing of the EOI advertisement.

11. The SACCOS reserves the right to accept or reject any bid, and to annul the Expression of Interest process and reject all bids at any time prior to short listing and awarding, without thereby incurring any liability to the affected bidder/s.

12. Further, through this solicitation Hazina SACCOS invites Expressions of Interest (EOI) from individuals and business entities, who are interested in investing in Hazina Business Centre at Njedengwa by providing their own proposals and business concepts that are congruent with the Dodoma Masterplan. All concepts are welcome as long as they align with the Dodoma City Masterplan.

13. The Bid will be available at the cost Equivalet to Usd 100 deposited in account number 20106600494 with NationalMicrofinance Bank (NMB) With a name Hazina SACCOS Ltd.

14. All applications should be submitted before **30th of November 2019.** The application should be submitted to:

**Chairman,**
**Hazina SACCOS Limited,**
**P.O. Box 9111,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**

Bidders are strongly encouraged to read the entire project business plan that can be obtained from Hazina SACCOS Ltd office located at Dodoma Hazina Saccos Ltd –Traesury square .

## HABARI MICHEZO

# DON O ZA SOKA
MA ZETI YA UL



# RONALDO: MESSI NDIYE KANIFANYA KUWA BORA

**Awali ya yote, unahitaji kipaji, vinginevyo huwezi kuwa zaidi, nisingeweza kuwa nilipo sasa pasipo...**

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo anaamini "ushindani wake mzuri" na straika wa Barcelon, Lionel Messi wakati akiwa LaLiga umemfanya kuwa mchezaji bora.

**Wote wawili wametwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka ya Ballon d'Or mara tano na wanachukuliwa kama wachezaji bora wa wakati wote.**

Ronaldo aliitumikia Real Madrid kwa miaka tisa kabla ya kujiunga na Juventus mwaka 2018 na Messi hivi karibuni alikiri walihitaji kuvumiliana kwa kila mmoja katika tuzo hiyo binafsi.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester United amekariri maoni hayo, akiliambia Jarida la France Football: "Watu wengi walisema kwamba tunalishana kila mmoja, kwamba kuwa pamoja nchini Hispania kunatufanya bora.

"Hilo pengine ni kweli. Nilihisi uwapo wake zaidi nikiwa Madrid kuliko nikiwa Manchester. Ulikuwa ushindani mzuri. Tulikuwa nembo ya klabu.

"Daima ni nzuri kusemwa kwa njia ya kupendeza. Ni vizuri ikiwa wanasema nimekuwa bora, mchezaji mzuri.

"Leo, ninasikia kila kitu wanachosema kuhusu mimi, lakini itakapokwisha, mwisho wa kazi yangu, sitajali kwa sababu nitafunga kwa kila kitu. "

Ronaldo anajulikana vizuri kwa kujitolea kwake mazoezini na kusisitiza kujituma zaidi uwanjani, kumemsaidia kuwa mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote.

"Awali ya yote, unahitaji kipaji, vinginevyo huwezi kuwa zaidi," alisema. "Hata hivyo, kipaji hakina maana bila kujituma zaidi.

"Nisingeweza kuwa nilipo sasa pasipo utamaduni wa kujituma zaidi."

Ronaldo hivi karibuni alifunga bao la 700 katika wasifu wake kisoka wakati Ureno ikichezea kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Ukraine, kati ya mabao hayo, 450 alifunga wakati akiitumikia miamba ya Santiago Bernabeu, Madrid.

Alipotakiwa kuchagua bao lake la kuvutia, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34, aliangukia katika bao lake la kubinjuka hewani mithili ya baiskeli iliyogeuzwa juu chini, aliloifungia Real Madrid kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Juventus msimu wa 2017-18.

"Kufikisha mabao 700 kunanifanya nijisikie fahari, ni idadi ya kuvutia ambayo wachezaji wachache wamefikisha," alisema.

"Kama nilipaswa kuchagua la kuvutia, ningeweza kusema moja dhidi ya Juventus kwa sababu ni bao ambalo nilikuwa nikijaribu namna ya kulifunga kwa miaka mingi."

## ZISIKUPITE

### BALE AIONYA REAL KUMUANIKA

NYOTA wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 30, ameitaka Real Madrid kutoanika kwa kuzichapisha rekodi zake za kimatibabu, kwa kutumia haki yake chini ya sheria ya Hispania ya ulinzi wa data binafsi.***(ESPN)***

### MILNER ANOGEWA LIVERPOOL

KIUNGO wa Liverpool, James Milner, 33, anataka kubaki klabuni hapo baada ya mkataba wake wa sasa ambao unamalizika mwishoni mwa msimu. ***(Guardian)***

### UTD KWA SOUMARE, DEMBELE

MANCHESTER United inavutiwa na kumwajiri kiungo wa Lille, Mfaransa Boubakary Soumare, 20, na straika wa Lyon, Moussa Dembele, 23. ***(ESPN)***

### VERTONGHEN AZUIWA INTER

TOTTENHAM imeiambia Inter haitamuuza beki wao, Jan Vertonghen, 32, katika dirisha la usajili la Januari lakini miamba hiyo ya Serie A inatumai nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji atajiunga nao akiwa huru majira ya joto. ***(Guardian)***

### XHAKA AFUATWA NYUMBANI

NAHODHA wa Arsenal, Granit Xhaka, 27, alitembelewa nyumbani na wachezaji watatu wa kikosi cha kwanza baada ya kuwajibu mbovu mashabiki wakati akizomewa alipofanyiwa mabadiliko ('sab') wakitoka sare nyumbani dhidi ya Crystal Palace Jumapili. ***(The Athletic)***

### ROMA YAMKATAA RODWELL

ROMA imekataa kumsajili kiungo wa Manchester City, Jack Rodwell, 28. ***(Corriere dello Sport, via Mail)***

### SMALLING KUREJEA UNITED

BEKI wa England, Chris Smalling, 29, anatarajia kurejea Manchester United pindi makataba wake wa mkopo wa mwaka mmoja utakapomalizika na Roma majira ya joto, licha ya tetesi za hivi karibuni za kutaka kujiunga jumla na klabu hiyo ya Italia. ***(Sky Sports)***

### SHEARER AMFUNGUKIA XHAKA

NAHODHA wa zamani wa England, Alan Shearer amesema Granit Xhaka anaweza kuhaha kurejea mchezoni baada ya kuonekana akitibuana na mashabiki wa Arsenal kufuatia kufanyiwa mabadiliko ('sab') wakati wa mechi dhidi ya Crystal Palace Jumapili. ***(Sun)***

### NAPOLI KUMKIMBIA HAALAND

NAPOLI itaondoa matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa RB Salzburg, mzaliwa wa Leeds, Erling Haaland katika dirisha la usajili la Januari kwa sababu wanatarajia Manchester United watamsajili kinda huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Corriere dello Sport, via Talksport)***

### MATIP NJE ZAIDI LIVERPOOL

BEKI wa Liverpool, Mcameroon Joel Matip, anajiandaa kuwa nje zaidi baada ya kuendelea kusumbuliwa na majeraha ya goti wakati akijiweka sawa kurejea na anaweza kuwa nje hadi wiki 6. ***(London Evening Standard)***

### KUITEMA SOUTHAMPTON

KIPA wa Southampton, Fraser Forster, 31, anayecheza kwa mkopo Celtic yupo tayari kukatwa sehemu ya malipo yake na miamba hiyo ya Ligi Kuu England ili kufanikisha kujiunga na klabu hiyo jumla. ***(The Scotsman)***

## Kipanga watambua wanapojikwaa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa timu ya Kipanga ya Ligi Kuu Zanzibar, Mohamed Khamis, amesema tatizo kubwa lililopo katika timu yao ambayo hadi sasa imeshinda mechi moja kati ya saba, ni mbinu za ufungaji jambo ambalo linasababisha kuendelea kupoteza mechi zao.

Kipanga ambayo tayari imeshuka dimbani mara saba msimu huu, imeshinda mechi moja ikitoka sare michezo mitatu na kupoteza tatu, hivyo kujikuta ikikalia nafasi ya 10 ikiwa na alama zake sita.

Akizungumza na gazeti hili jana kocha huyo alisema bado wachezaji wake wanatakiwa kupata mazoezi ya umakini katika upachikaji wa mabao ili kuondoa changamoto ya kosakosa kama ilivyo hivi sasa.

Alisema tayari wameshaanza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya mzunguko wa nane, ambapo Kipanga itakuwa ugenini Kisiwani Pemba kupepetana na timu ya Machomane.

"Bado hatujapata matokea mazuri sana tangu kuanza kwa ligi, na tayari tumeshaanza mazoezi ya mapungufu tulio nayo ikiwamo safu nzima ya ushambuliaji, walinzi na hasa mabeki wa kati ambao muda mwingine wanapangulika ovyo uwanjani," alisema.

Kwa upande wake nahodha wa Kipanga, Imani Abdullahi, alikiri kuwapo kwa changamoto ya umaliziaji katika kikosi chao licha ya kucheza vizuri.

## Shimmuta kurindima Mwanza Novemba 17

**Na Shufaa Lyimo**

MICHUANO ya Mashirika ya Umma na Kampuni Binafsi (Shimmuta), inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Novemba 17 hadi Desemba Mosi, mwaka huu, jijini Mwanza.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mwenyekiti wa Shimmuta, Khamis Mkanachi alisema maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano yetu ya Mwanza yanaendelea vizuri kila taasisi inafanya mazoezi kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano hiyo," alisema.

Aidha, alisema katika mtanange huo kutakuwa na michezo mbalimbali ikiwamo riadha, kukimbiza kuku, mpira wa miguu, kuruka kamba na mingine mingi.

"Kutakuwa na michezo mingi siku hiyo si tu mpira wa miguu tunaomba wadau mbalimbali wajitokeze kwa wingi kushuhudia mashindano hayo ambayo mwaka huu tumeyaboresha kwa kiasi kikubwa," alisema mwenyekiti huyo huku akiwataka Watanzania kupenda kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara kwa kuwa michezo ni afya.

# KAGERE: POINTI 3 KWANZA, MFUNGAJI KWETU BAADAYE

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa soka wakiwa na kiu ya kuona Meddie Kagere akiendeleza kasi yake ya kucheka na nyavu katika mechi ya leo dhidi ya Mwadui FC, mshambuliaji huyo aliyefunga mechi tano mfululizo, amesema anachotazama ni ushindi wa timu na si yeye kufunga.

Kagere ambaye ameichezea Simba mechi zote sita msimu huu, amefunga mabao saba katika michezo mitano mfululizo kabla ya mchezo dhidi ya Singida United kushindwa kucheka na nyavu wakati Miraji Athumani akiifungia timu hiyo bao pekee liliwafanya kuibuka ushindi wa bao 1-0 katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha mwishoni mwa wiki.

**Simba ambayo ilitua juzi mjini Shinyanga, itashuka katika Uwanja wa Kambarage leo saa 10 jioni kumenyana na Mwadui FC, ikiwa imeshinda mechi zake zote msimu huu wakati huu ikiwa kileleni mwa ligi hiyo.**

Hata hivyo, Kagere ambaye yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu, amesema kushindwa kufunga katika mchezo mmoja kwake si tatizo na kwamba jambo la muhimu kwake ni timu kuvuna pointi tatu.

"Huna tatizo kwangu kufunga au kutokufunga, la muhimu, tunachotazama wachezaji wote kwetu ni timu kupata pointi tatu, hilo ndilo jambo la muhimu, mengine yatafuata," Kagere alisema.

Msimu uliopita, Kagere alitwaa Kiatu cha Dhahabu baada ya kuibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara na hadi sasa ndiye anayeiongoza mbio hizo akiwa na mabao saba, matatu mbele ya mshambuliaji mwenza wa Simba, Miraji ambaye anashika nafasi ya pili huku wachezaji wengine wakifuata nyuma wakiwa wamecheka na nyavu mara tatu tu.




Mchezaji wa timu ya Kituo cha JKM, Ally Abeid, akijaribu kumtoka mchezaji wa timu ya Kituo cha Fountain Gate, Mwinyi Daud (kushoto) katika mchezo wa mashindano ya U-17 uliochezwa katika viwanja vya Jakaya Kikwete mwishoni mwa wiki. JKM Park ilishinda kwa bao 1-0 na kufuzu nusu fainali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mwambusi afunguka City ikiibanjua Mbao*

**Na Focus Nicus**

BAADA ya Mbeya City kuzinduka na kupata ushindi wa ugenini wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji, Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, imesema sasa kazi imeanza rasmi.

Huo ni ushindi wa kwanza kwa Mbeya City msimu huu baada ya kushuka dimbani mara saba ikitoka sare nne na kupoteza mechi mbili.

Kocha wa Mbeya City, Juma Mwambusi alisema kikosi chake kimeanza kuimarika na kuelewana, hivyo ana uhakika wa kuendelea kukisuka vema na kuweza kuendeleza ushindi walioanza kuupata juzi.

"Wachezaji wangu wameanza kuelewana, bado ninaendelea kukiandaa ili kuweza kurudia makali yake na kuendeleza ushindi," alisema.

Katika mchezo huo uliochezeshwa na refa Martin Saanya wa Morogoro akisaidiwa na Sunday Kamba pamoja na Abdulaziz Ally wote kutoka Arusha, Mbao FC ilianza kuchezea kichapo dakika ya kwanza tu baada ya kuanza kipindi cha pili, kufuatia mchezaji wake, Babilas Chitembe kumchezea rafu Baraka Ngusa ndani ya 18 na kuzaa penalti iliyozamishwa kimyani na Peter Mapunda dakika ya 48.

Kama mshambuliaji Said Khamis Junior angetulia na kuongeza umakini, angeweza kuisawazishia Mbao FC, lakini mkwaju wake wa penalti uliokolewa na kipa Haroun Mandanda dakika ya 88 kufuatia Datus Peter kuchezewa rafu na beki wa Mbeya City, Hassan Mwasapili.

Na katika dakika ya 90 wakati wengi wakiamini Mbeya City itaibuka na ushindi wa bao 1-0, Emmanuel Charles Lukinda alisawazishia Mbao FC dakika ya 90 na wakati mashabiki wa timu hiyo hawajamaliza kushangilia, Peter Mapunda akaifungia Mbeya City bao la ushindi kwa shuti la mpira wa adhabu dakika ya majeruhi.

# Michezo

Jumatano Oktoba 30, 2019
Nipashe



Ronaldo: Messi kanifanya kuwa bora UKURASA 30

SHUGHULI LEO...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini jana katika Uwanja wa CCM Kambarage mjini Shinyanga kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mwadui FC itakayopigwa uwanjani hapo leo. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# ZAHERA AISHUKIA YANGA KUTIMULIWA

## ●●● Asema alisajili kwa ajili ya Ligi Kuu na si kimataifa huku akidai Pyramids si saizi yao, Ally Mayay aionya...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa Yanga wakitaka Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera sasa atimuliwe huku uongozi wa timu hiyo, ukieleza umesikia "kilio" chao, na kwamba unasubiri kwanza ripoti ya kiufundi ambayo ndio itatoa mwongozo, Mkongomani huyo ameishukia klabu hiyo na kumwaga kila kitu hadharani huku akieleza wamesajili wachezaji wa Ligi Kuu tu na si wa kimataifa.

**Kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Pyramids ya Misri kwenye mechi ya mchujo ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba mwishoni mwa wiki, ndicho kilichowaibua mashabiki wa Yanga wakitaka Zahera atimuliwe.**

Baadhi ya sababu ya mashabiki hao kutaka Zahera atimuliwe ni kutokana na timu kushindwa kuwa na muunganiko mzuri, kucheza ovyo pasipo maelewano, lakini wakieleza zaidi ya asilimia 90 ya wachezaji wote waliosajiliwa ni kutokana na mapendekezo yake, hivyo kufanya vibaya kwa timu lazima abebe mzigo huo kwa kutimuliwa.

Lakini juzi, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, aliliambia Nipashe kuwa uongozi ulisikia "kilio" cha mashabiki wao, ila uamuzi wa kuachana na Zahera, bado haujazungumzwa na kwamba wanasubiri ripoti ya kiufundi ambayo ndio itatoa mwongozo wa hatima yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema kikosi cha Yanga hakina mchezaji anayeweza kupambana na timu kubwa za kimataifa na wao walisajiliwa na kuandaliwa kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara tu.

Zahera alisema hakushangazwa na hajaumizwa na matokeo yaliyopatikana katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na "maneno" ya mashabiki hayamuumizi kichwa.

"Mimi ni kocha mwenye uzoefu mkubwa hapa barani Afrika, Yanga haina mchezaji hata mmoja mwenye hadhi ya kucheza Pyramids, hatukusajili wachezaji wa kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hatukujiandaa na mashindano hayo, sisi tulisajili kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, hatukuwa tayari kupambana," alisema Zahera. Aliongeza kuwa mashabiki wa Yanga wanatakiwa kuumia endapo watafungwa na klabu kutoka Burundi au Uganda na kamwe wasiumie pale wanapofungwa na timu kama Pyramids ambayo imejipanga na kujiandaa vema kupambana katika mashindano haya ya kimataifa.

"Mimi nilijiandaa kwa Ligi Kuu tu, nikiwa Afcon (Kombe la Mataifa Afrika), ndio nikaelezwa Yanga tunashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wachezaji tulionao ni wa kawaida, nasema hatukuwa tayari kushiriki mashindano hayo," alisisitiza kocha huyo Mmsaidizi wa zamani wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambaye mkataba wake na Yanga unatarajiwa kumalizia Septemba mwakani.

Aidha, Zahera alisema pia hana hofu ya kutimuliwa na vitendo vya kurushiwa chupa au kuzomewa na mashabiki ni vya kawaida kwenye maisha ya mpira wa miguu.

Wakati Zahera akieleza hivyo, mchambuzi wa soka nchini na Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Yanga aliyewahi kuitumikia klabu hiyo kwa mafanikio makubwa, Ally Mayay ameionya klabu hiyo akiitaka kuwa makini kwa maamuzi watakayoyafanya kuhusu kumtimua kocha huyo.

Mayay alisema ni kweli kwa sasa Yanga inacheza soka bovu ukilinganisha na msimu uliopita ikiwa na kocha huyo huyo ambaye kabla ya msimu kuanza alipewa nafasi ya kufanya usajili wa wachezaji anaowataka tofauti na aliowakuta msimu uliopita.

"Kwa zaidi ya asilimia 90 wachezaji waliopo Yanga ni kocha ndiye aliyependekeza wasajiliwe, hivyo mashabiki ni wazi walitegemea kuiona Yanga bora tofauti na ilivyo sasa, kinachoonekana ni timu kukosa muunganiko mzuri kwa sasa," Mayay alisema.

"Lakini suala la kumtimua Zahera kwa sasa linapaswa kufanywa kisayansi zaidi na kwa umakini wa hali ya juu kwani ni katikati ya msimu na ligi inaendelea hivyo kufanya mabadiliko kwa sasa, kunaweza kuharibu kila kitu."

## Kagere aishika Shy, Aussems afunguka

**Na Somoe Ng'itu,** SHINYANGA

KAGERE, Kagere, 'This is Simbaaaa, This is Simbaaaa! Ndio maneno yaliyokuwa yanatamkwa na wanachama na mashabiki wakati wanaipokea timu yao ya Simba ambayo wataishuhudia ikishuka kuwakabili Mwadui FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mjini hapa.

Mshambuliaji wa kimataifa wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara Mnyarwanda Meddie Kagere na Miraji Athumani, wanatarajiwa kuongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo inayoongoza katika msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema wamekuja kushindana kama ambavyo walifanya katika mechi zilizopita za ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Aussems alisema wanatarajia kukutana na changamoto kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri na kujiweka kwenye nafasi nzuri na kutimiza malengo iliyojiwekea katika msimu huu.

"Tunatarajia kufanya mazoezi ya mwisho leo (jana) jioni, matumaini yetu ni kuwa na mchezo mzuri, lakini wenye changamoto na ushindani, hakuna mechi rahisi, timu zote zinajiandaa kusaka matokeo mazuri, na wachezaji wanajua ni nafasi yao ya kujitangaza na kuonyesha wanaweza," alisema Aussems.

Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, alisema jana kuwa kikosi chake kiko imara na kimefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo wa leo.

"Tunaijua Simba, tunajua wachezaji wake wanavyocheza, tumejiandaa kuwashangaza, tumepanga kuisimamisha, tunawaomba mashabiki wetu wajitokeze kutushangilia katika mechi hii ya kesho (leo)," Khalid aliliambia gazeti hili jana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >